



Jarida la NEMC



HALIUZWI

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 006 | JANUARI - MACHI, 2022

MAKAMU WA RAIS AZINDUA SERA YA MAZINGIRA



Ndani:

👉 “UMUHIMU WA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA (TAM) NA UANDAAJI WA MPANGO WA USIMAMIZI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA PALE MGODI UNAPOANZISHWA NA UNAPOFUNGWA .” - DKT. GWAMAKA

👉 UPANDAJI WA MITI KWENYE MAZINGIRA YETU NI NJIA MOJAWAPO YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO YA HEWA YA UKAA - MHE. JAFO

👉 **MAKALA:** FAHAMU FURSA NA CHANGAMOTO ZA TAKA NGUMU MKOA WA DAR ES SALAAM

📷 @nemctanzania

📺 NemcTVTanzania

🌐 www.nemc.or.tz

#MazingiraYetuUhaiWetu



BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira;
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.

BODI YA UHARIRI:

Mwenyekiti: Dkt. Menan Jangu
Mhariri Mkuu: Irene John

Wachangiaji:
Monica Sapanjo
Dalia Charles
Rose Mtui
Rashda Swedi
Adam Sayi
Judith Mwakolo

Msanifu Michoro:
Blasius Haule

Na.	Maelezo	Uk
1.	MHE. MAKAMU WA RAIS AZINDUA SERA YA MAZINGIRA	3
2.	UPANDAJI WA MITI KWENYE MAZINGIRA YETU NI NJIA MOJA WAPO YA KUKABILIANA NA ATHARI YA HEWA YA UKAA - MHE. JAFO	4
3.	KIWANDA CHA GUOYANG CHAPEWA MIEZI SITA KUKAMILISHA MCHAKATO WA KUPATA CHETI CHA UKAGUZI WA MAZINGIRA (ENVIRONMENTAL AUDIT CERTIFICATE).	5
4.	MAKALA: ADA NA TOZO ZA MAZINGIRA	6
5.	MSINGI BORA WA UTUNZAJI WA MAZINGIRA UANZIE NGAZI YA WATOTO - DKT. JAFO	7
6.	NEMC YATOA SIKU TATU KWA DEREVA WA GARI LILILOMWAGA KEMIKALI MIKUMI	7
7.	UMUHIMU WA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA (TAM) NA UANDAAJI WA MPANGO WA USIMAMIZI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA PALE MGODI UNAPOANZISHWA NA UNAPOFUNGWA . - DKT. GWAMAKA	9
8.	MAKALA: UHARIBIFU VYANZO VYA MAJI NA ATHARI ZAKE	10
9.	TUSHIRIKIANE KWA KARIBU KATIKA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZA KIMAZINGIRA- MHE. KHAMIS	11
10.	UZINDUZI RASMI WA MRADI WA UHIMILI WA MABADILIKO YA TABIANCHI - PWANI ZA ZANZIBAR	12
11.	WAZIRI JAFO AAGIZA KILA MWANAFUNZI KUPANDA MTI NA KUUTUNZA	12
12.	MAKALA: ATHARI ZA UCHAFUZI WA MAZINGIRA ZITOKANAZO NA KELELE	13
13.	WAZIRI JAFO AZINDUA BODI YA NEMC JIJINI DODOMA	14
14.	MAKALA: FAHAMU FURSA NA CHANGAMOTO ZA TAKA NGUMU MKOA WA DAR ES SALAAM	15
15.	MAKALA: ATHARI ZA MAZINGIRA KATIKA MAENEO YA MIGODI	16
16.	MAKALA: CHANGAMOTO YA MAGUGU MAJI ZIWA BABATI KUTATULIWA	18
17.	HABARI PICHA	20
18.	HABARI PICHA: MAONESHU YA KIMATAIFA YA MAZINGIRA - QATAR (10 - 14 Machi, 2022)	22
19.	KAULI YA MAZINGIRA	24
18.	KAULI YA MAZINGIRA: KATUNI	26

MAKAMU WA RAIS AZINDUA SERA YA MAZINGIRA


Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango alikuwa Mgeni rasmi katika uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 iliyozinduliwa tarehe 12 Februari, 2022 Jijini Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa Habari Jijini Dodoma, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga alisema Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 imejumuisha masuala ya mazingira yaliyokuwemo katika Sera ya 1997 na masuala mapya.

Masuala mapya katika Sera mpya ya mwaka 2021 ni pamoja na:

1. Udhhibiti wa taka za kielektroniki,
2. Usimamizi na matumizi ya kemikali, na
3. Udhhibiti wa uchafuzi katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi.

Masuala mengine ni pamoja



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango akikabidhiwa kitabu cha Muongozo wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo Uzinguzi huo uliyofanyika jijini Dodoma.

na Mabadiliko ya tabianchi; Usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa; na Udhhibiti wa viumbe vamizi.

"Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 imeongeza wigo wa masuala na changamoto za mazingira zinazopaswa kufanyiwa kazi katika kipindi husika, ili kuleta maendeleo endelevu vilevile Sera mpya imezingatia changamoto mpya za kimazingira zinazoendelea kujitokeza kutokana na mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi, kijamii na kimazingira yanayoendelea duniani" Alisisitiza Bi. Mary Maganga.

Amesema kuwa, Serikali imeamua kuwa na Wiki ya Uzinduzi wa Sera itakayoanza tarehe 07-12/02/2022 ambayo itaambatana na shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira ikiwa ni sehemu ya masuala ya msingi yanayoelekezwa katika Sera mpya.

Bi. Maganga amezitaja shughuli zitakazofanyika katika wiki hiyo kuwa ni Upandaji miti Jijini Dodoma katika maeneo ya Medeli, Iyumbu, Ileni na maeneo ya barabara inayoanzia Chimwaga, Chuo Kikuu cha Dodoma kuelekea barabara ya Dodoma Dar es Salaam. Aidha, Kufanya usafi pembezoni mwa barabara inayoanzia Shule ya Martin Luther hadi Wajenzi kupitia Nzuguni, Ilazo, Ipagala na Area C; Kutoa elimu kuhusu utenganishaji wa taka, kufanya Usafi katika soko la Changombe pamoja na Utoaji wa Elimu ya Mazingira kwa wananchi na wadau kupita vyombo vya habari.

Dhumuni la kuwepo kwa shughuli hizo ni kurejesha hali ya asili ya mazingira iliyoharibika kutokana na shughuli za kibinadamu kwa kuwa na zoezi la upandaji miti, kuboresha afya ya jamii na utoaji elimu ya utenganishaji taka kwa ajili ya udhibiti wa taka ngumu na kuwezesha urejelezaji wa taka kwenye bidhaa na huduma mbalimbali.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango akipanda mti siku ya uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 uliyofanyika jijini Dodoma.

UPANDAJI WA MITI KWENYE MAZINGIRA YETU NI NJIA MOJAWAPO YA KUKABILIANA NA ATHARI YA HEWA YA UKAA - MHE. JAFU



Waziri wa nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dkt. Seleman Jafo amewataka wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi za misitu kuendelea na utamaduni wa utunzaji wa mazingira katika maeneo hayo ili kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi.

Waziri Jafo ameyasema hayo baada ya kutembelea Msitu wa Pugu Kazimzumbwi ulioko Wilayani Kisarawe mkoa wa Pwani, kuona namna ambavyo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ilivyojidhatiti kuendeleza msitu huo kama sehemu ya kuhifadhi mazingira.

Aidha ameelekeza kila halmashauri ianze programu ya kutumia mvua zinazoendelea kunyesha nchini kupanda miti ili kuweza kufikia lengo la miti milioni 276 kwa mwaka alisisitiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusimamia zoezi hilo.

Waziri wa nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dkt. Seleman Jafo akizungumza jambo mara baada ya kutembelea Msitu wa Pugu Kazimzumbwi ulioko wilayani Kisarawe mkoa wa Pwani, kuona namna ambavyo Wakala wa huduma za Misitu Tanzania (TFS) ilivyojidhatiti kuendeleza msitu huo kama sehemu ya kuhifadhi mazingira.

Amesema upandaji wa miti kwa wingi kwenye mazingira ni njia mojawapo itakayosaidia kukabiliana na changamoto za hewa ukaa inayoweza kuhatarisha maisha ya mwanadamu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka amesema kuna umuhimu wa utunzaji wa mazingira hivyo watanzia wanatakiwa kuweka mazingira yao kama yalivyokuwa awali na vilevile watanzia wakiendelea kupanda miti kwa wingi basi nchi itakuwa imejawa na misitu na tutaweza kupunguza athari kubwa tunazozipata kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Nae Kamanda wa Kanda ya Mashariki

TFS, Kamishna Msaidizi Caroline Malundo amesema msitu wa Pugu Kazimzumbwi ni moja ya hifadhi ya msitu muhimu uliopo hapo Wilayani Kisarawe ambao umekuwa ukichochea Utalii wa ndani kutokana na mikakati iliyowekwa na Wakala wa Misitu TFS.

“Tunafahamu kila Halmashauri imepewa mwongozo wa uwekaji wa vitalu kwa lengo la kusaidia katika maeneo mbalimbali hasa katika taasisi, tunataka tuone katika shule zetu zote, vituo vya afya, hospitali maeneo hayo yote yanapandwa miti”.

Alisema Mhe. Jafo

KIWANDA CHA GUOYANG CHAPEWA MIEZI SITA KUKAMILISHA MCHAKATO WA KUPATA CHETI CHA UKAGUZI WA MAZINGIRA (ENVIRONMENTAL AUDIT CERTIFICATE).



Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka (Kushoto) akiongea na msimamizi wa kiwanda cha Guoyang Biotech Company Mr. Liu Xi Shuang wakati alipofanya ziara kiwandani hapo.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka amemtaka mmiliki wa kiwanda cha Guoyang Biotech Company Ltd kilichopo katika Mtaa wa Kiboga, Kata ya Msongole, Wilayani Ilala kuhakikisha ndani ya miezi sita wawe wamekamilisha mchakato wa kupata cheti cha ukaguzi wa mazingira (Environmental Audit Certificate).

Ameyasema hayo alipokuwa katika ziara ya kukagua masuala yote yanayohusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika kiwanda hicho ambacho kinalalamikiwa na wakazi wa eneo hilo kwa kusababisha harufu kali ambayo imekuwa tishio kwa wakazi wa eneo hilo.

Kiwanda hicho kinahusika na



Bwawa la kuhifadhia mafuta machafu katika kiwanda hicho.

utengenezaji wa mafuta ya dizeli ya viwandani (Industrial Diesel) lakini inasemekana kuwa mafuta hayo huuzwa kwa wenye vituo vya mafuta kwa hiyo NEMC katika ziara hiyo ilikua ikifuatilia kuhusu malalamiko hayo.

“Mafuta yanayozalishwa hapa hayafai kutumika kwenye vituo vya mafuta kwa sababu yana viasili vingi visivyofaa ambavyo vikiingia kwenye mafuta husababisha injini kuwa na umri mfupi na kuharibika kwa haraka, nawatahadharisha wenye

vituo wasije kununua mafuta haya” Dkt. Gwamaka

Naye Kaimu Meneja wa Kanda ya Mashariki kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Bw. Emmanuel Lewanga alisema kuwa wako na NEMC katika ziara hiyo ya kutembelea kiwanda tajwa na wao watachukua sampuli ya mafuta ya dizeli inayozalishwa kiwandani hapo, na kuipeleka maabara kuifanyia uchunguzi kujua kemikali ya aina gani inachanganywa kwenye mafuta hayo machafu.

ADA NA TOZO ZA MAZINGIRA

Utangulizi

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na Kanuni ya Ada na Tozo za Mazingira ya 2021. Wadau mbalimbali wa Mazingira wameelimishwa kuhusu wajibu wa kuhifadhi na kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na kulipa ada na tozo za mazingira. Zoezi la uelimishaji limehusisha Ofisi zote za Baraza ikiwa ni pamoja na Makao Makuu na Ofisi za Kanda tisa (9).

Ikumbukwe kuwa Baraza linajijendesha katika kusimamia majukumu yake ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa kutumia fedha zitokanazo na Ada na Tozo mbalimbali za Mazingira. Hii ikiwa ni kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004. Tozo zitumikazo kwa sasa zimeainishwa katika Kanuni ya Ada na Tozo za Mazingira ya mwaka 2021 katika toleo la Serikali namba 387 lililochapishwa tarehe 14/05/2021. Tozo hizo za Mazingira zinahusisha shughuli zote zinazoendelea na zinazotarajia kuanza kama ambavyo Kanuni imeainisha.

Ada na tozo ya mazingira maana yake ni kiwango cha pesa kinacholipwa au kinachotowza na Baraza kwa ajili ya kuwezesha kufanya mapitio ya Tathmini za athari kwa Mazingira, na vilevile ufuatiliaji na uhakiki wa mazingira kama ilivyoainishwa katika Sheria ya mazingira ya mwaka 2004. Ada hizi hulipwa na (miradi yote iliyoainishwa kwenye kanuni pamoja watalamu washauri wa mazingira) kila mwaka wa fedha wa Serikali. Tozo zimeainisha aina ya miradi na viwango vyake. Aidha, tozo zingine zinatowza kutokana na kutozingatia viwango na kanuni za mazingira, pamoja na vibali maalumu vitolewavyo na Baraza.

Baraza limepewa jukumu na mamlaka kisheria kufuatilia na kuhakiki uzingatiaji wa viwango vya mazingira kwa miradi yote inayoanzishwa nchini. Katika kutekeleza jukumu na mamlaka hayo inategemeana na rasilimali watu na fedha. Mwanzoni Baraza lilitegemea sana ufadhili kutoka kwa wadau wa maendeleo na ruzuku kidogo kutoka Serikalini ili kutekeleza majukumu yake. Mwaka 2008, Bunge liliridhia kanuni za ada na tozo za mazingira ilianzishwa ikiainisha miradi yote inayochafua /kuharibu mazingira kulipa ada na tozo za mazingira kulingana na aina ya mradi. Kwa sasa mchakato huu unasimamiwa na Kanuni ya Tozo za Mazingira ya Mwaka 2021 (Environmental Management (Fees and Charges) Regulations, 2021)

Matakwa ya Kisheria Kuhusu Ada na Tozo

Viwango vya Tozo vimeainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Kifungu Na 230(2) (b) iliyotengeneza Kanuni ya Ada na Tozo ya mwaka 2021. Hii inahusisha Ada na Tozo za mwaka, Usajili wa Miradi, Gharama za mapitio ya miradi na faini (penalty). Aidha, Sehemu ya Sita ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 yenye Kifungu cha 81 hadi cha 103 inaelekeza kila shughuli ya maendeleo ifanyiwe Tathmini ya Athari kwa Mazingira na inatoa ufafanuzi wa hatua za kufuata. Vilevile Sheria imeainisha jukumu la mwekezaji la gharama za kulipia kwa ajili ya mapitio ya Taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM).

Kwa mara ya kwanza Kanuni ya Tozo ilianzishwa mwaka 2008 na ilianza kutumika mwaka wa fedha wa 2012/2013. Baraza linafahamisha kuwa Kanuni za Tozo zimefanyiwa marejeo mara kadhaa tangu Kanuni za tozo kuundwa mwaka 2008. Kanuni hizo zilifanyiwa mabadiliko mwaka 2016 na Mwaka 2018, Mwaka 2019 na Mwaka 2021 ikiwa ni katika mustakabali wa kutekeleza Mwongozo wa Serikali wa kuboresha Mazingira ya Uwekezaji nchini (Blue Print on Regulatory Reform to Improve Business Environment in Tanzania). Hata hivyo, Kanuni za Ada na Tozo za mwaka 2019 ziliiboreshwa kufuatia mabadiliko yaliyofanyika kwenye Kanuni za Taka Hatarishi za Mwaka 2021. Viwango vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Ada na Tozo zilitakiwa kuwiana na shughuli zinazofanyika kwenye usimamizi wa taka hatarishi ikiwa ni pamoja na ukusanyaji, usafirishaji na utunzaji.

Gharama za Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM)

Baraza kwa nyakati tofauti limelazimu kutoa ufafanuzi juu ya aina mbalimbali za tozo kwani wadau wamekuwa wakishindwa kutenganisha gharama za mapitio zinazolipwa NEMC na zile za ufanyaji TAM na uandaaji wa andiko zinazitakiwa kulipwa kwa mtaalam elekezi. Gharama za TAM ziko kwenye makundi makuu mawili: 1) Gharama za moja kwa moja za mradi na 2) Gharama za mapitio ya mradi (ada za NEMC kama zilivyoainishwa kwenye Kanuni).

Gharama za mradi zinategemea mambo kadhaa ikijumuisha: 1) Eneo ambapo mradi upo (makazi ya watu, kwenye hifadhi, kwenye mkondo au chanzo cha maji; 2) Ukubwa na shughuli mbalimbali zinazohusu mradi; 3) Changamoto za kimazingira na kijamii zinazoweza kujitokeza kutokana na uanzishaji wa mradi; 4) Aina ya mradi (mgodi, kiwanda cha utengenezaji wa kemikali na 5) Taswira ya mradi kwa mamlaka husika na jamii



Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka
Mkurugenzi Mkuu wa NEMC

inayozunguka eneo la mradi kwa ujumla

Gharama za moja kwa moja za TAM kwa wataalamu elekezi ni zile gharama za mchakato mzima wa uandaaji wa andiko la TAM ambazo hulipwa moja kwa moja kwa mtaalamu elekezi. Gharama hizi zinajumuisha mambo kadhaa kulingana na mchakato ulivyo. Mara nyingi gharama hizi hujumuisha gharama za utaalumu wa ufanyaji tathmini, uchukuaji na upimaji wa sampuli na uandaaji wa andiko na pia gharama za usafiri na malazi ukusanyaji wa taarifa mbalimbali. Gharama za TAM ni suala la makubaliano baina ya mteja na mtaalam wa TAM.

Muda wa Ulipaji Ada na Tozo za Mazingira

Tozo za Mazingira za Mwaka hutakiwa kulipwa katika kipindi cha kuanzia tarehe 1/7 hadi Tarehe 31/12 ya kila mwaka wa fedha kwa mujibu wa Sheria. Aidha ucheleweshaji wa ulipaji wa Tozo baada ya tarehe 31/12, zitalipwa na penati ya 5% kwa kila mwezi ambao umepitishwa. Kuhusu malipo ya mapitio ya Tathmini za Athari za Mazingira na Ukaguzi, Baraza litatoa Hati ya Madai (Invoice) na Kumbukumbu Namba ya Malipo (Control Number) inayoonesha kiwango cha gharama za mapitio ya tathmini kinachotakiwa kulipwa kutokana na Kanuni ya ada na Tozo ya Mwaka 2021. Kiasi hicho kinatakiwa kilipwe kabla au wakati wa uwasilishaji wa Taarifa ya Tathmini ya Athari ya Mazingira au Taarifa ya Ukaguzi wa Mazingira. Gharama hizo zinatofautiana kulingana na mradi husika.


Vilevile wamiliki wa miradi wanatakiwa kutoa taarifa Baraza pale ambapo miradi yao itakuwa imefikia ukomo wa utekelezaji ili Baraza liweze kujiridhisha kama wametokeleza Sheria ya mazingira kama vile kulipa Ada na Tozo mbalimbali pamoja na kuhakikisha, matakwa ya kurekebisha hali ya mazingira yamezingatiwa katika uhitimishaji wa utekelezaji wa miradi.

Huduma kutoka katika Ofisi za Kanda

Katika kuhakikisha huduma kwa jamii zimesogezwa, Baraza limeanzisha ofisi za kanda.

Inaendelea Uk. 08 >>>

MSINGI BORA WA UTUNZAJI WA MAZINGIRA UANZIE NGAZI YA WATOTO - DKT. JAFU



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Selemani Jafo akipanda mti wakati wa uzinduzi wa kampeni ya soma na mti iliyofanyika katika shule ya msingi Sinza Jijini Dar es Salaam.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo amewaelekeza wakuu wa Mikoa, Wilaya na maafisa mazingira wote kuendelea kusimamia ajenda ya usafi wa mazingira na kuisisitiza kuwa kila mwanafunzi apande mti mmoja kwani ndio msingi bora wa utunzaji wa mazingira.

Aliyasema hayo alipokuwa anazindua rasmi kampeni ya upandaji miti katika shule ya msingi Sinza iliyopo Wilaya ya Ubungo, Mkoa Dar es Salaam. Aliendelea kusema kuwa maelekezo ya Rais mama Samia Suluhu Hassan ya upandaji miti, utunzaji wa mazingira na ufanyaji wa usafi lazima yafanyike kwa nguvu zote kwani Rais amepata heshima kubwa duniani hasa ya kimazingira kama Serengeti, Ngorongoro nk. Ambayo wengine hawana lakini pia nchi imeweka kielelezo kutengeneza miradi ambayo inajali mazingira kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

"Watanzania wenzangu tujali sana ajenda ya mazingira na tupambane na mabadiliko ya tabianchi, natumia fursa hii kuwaomba Watanzania na walimu wote twendeni tukapande miti. Tukipandakiza ajenda hii kwa watoto watakuwa na ajenda ya kutunza mazingira katika maisha yao yote. Tuna Halmashauri 184 na maelekezo ya Serikali ni lazima kila Halmashauri ipande miti mil. 1.5, wataalamu wa misitu kutoka TFS wanasema asilimia 62 huwa inastawi na lengo hilo likitimia tutaifanya Nchi yetu iwe ya kijani na Tanzania itakuwa salama." - alisema Dkt. Jafo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Bw. Herry James alisema kuwa Wilaya ya Ubungo inatekeleza kwa viwango maelekezo ya Serikali lakini pia inajali na kuheshimu mahitaji na maslahi ya wananchi wote ili kuwahudumia kwa uzuri na usalama ni lazima mazingira yao yawe safi wakati wote.

"Sisi kama wana Ubungo tumepokea kampeni ya upandaji miti kwa mikono miwili. Na swala la utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti tutarithisha kuanzia kwa watoto shule, mtoto huyu ambaye yupo darasa la kwanza akikabidhiwa mti wake chini ya kampeni hii maana yake atamwagilia kwa kuutunza kwa miaka saba, siku anahitimu anapatiwa cheti cha kuhitimu na atakuwa anatukabidhi mti wetu alioutunza kwa miaka saba. Program ikisimamiwa vizuri tunao uhakika wa kuwa na miti ya kutosha na iliyotunzwa vizuri." - alisema Bw. Herry.

Naye meneja wa Kanda ya Kaskazini Mashariki kutoka NEMC Bw. Arnold Mapinduzi amesema kama NEMC wameshiriki katika uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti ambao umeandaliwa na mabalizi wa mazingira lakini kama NEMC watakuwa wanakagua na kuhakikisha miti inakuwa na inaishi. Lakini kubwa ni kuwekeza kwa watoto kunakuwa na uhakika zaidi wa uendeleu kwa familia na jamii kwa ujumla.

Balizi wa Mazingira Bw. Peter Niboye amesema kama mabalizi wamejipanga kufanya kampeni hii ya upandaji miti nchi nzima na wapo tayari kupokea maelekezo na litakuwa ni zoezi endelevu.

NEMC IMETOA SIKU TATU KWA DEREVA WA GARI LILILOMWAGA KEMIKALI MIKUMI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitoa muda wa siku tatu kwa dereva wa gari lililomwaga kemikali aina ya Sulphur katika eneo la Msimba Tarafa ya Mikumi Wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro, kujisalimisha mara moja katika ofisi za NEMC zilizopo Morogoro mjini kwani kemikali hizo zimeanza kuleta madhara kwa wananchi waliokaribu na eneo hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Ndg. Jamal Baruti alitoa siku hizo baada ya kufika na kujionea namna wananchi wa eneo hilo walivyoathiriwa na kadhia hiyo.

NEMC ilifikia hatua hiyo baada ya kupata taarifa ya kutokea kwa tukio hilo, huku wananchi wakianza kupata madhara ikiwemo kuumwa macho, vichwa pamoja na kuwashwa kwa ngozi.

Ndg. Baruti alisema NEMC imesikitishwa na kitendo cha dereva wa gari hilo aliyekuwa akitokea Dar es Salaam kuelekea nchi ya jirani ya Kongo kumwaga kemikali na kutokomea kusikojulikana huku ikiwa bado haijafahamika chanzo cha kuwepo kwa Sulphur hiyo kama ni ajali ama laa.

Katika hatua nyingine NEMC inamfuatilia ili kumchukulia hatua dereva kwa kutokufuata Sheria ya Mazingira, kwani kitendo alichokifanya ni uharibifu wa mazingira huku wahanga wakubwa wakiwa ni wananchi wanaoishi jirani na eneo hilo kwani Kemikali hiyo ina madhara makubwa kwa binadamu na mazingira kwa ujumla.

Sambamba na hayo NEMC ilitoa rai kwa madereva wanaoendesha magari ya mizigo hususani wanaobeba kemikali kufuata Kanuni na miongozo ya ufungaji wa mizigo pamoja na kutumia vifungashio vinavyokidhi vigezo.

Kwa upande wao wananchi ambao ni mashuhuda wa tukio walisema gari hilo lilidondosha kemikali hizo usiku wa Januari mosi 2022 na kusababisha madhara kwa wananchi ikiwemo kuumwa na vichwa, macho na kifua hali ambayo ilileta sintofahamu kwa wakazi hao kwa kuhofia afya zao na kutokujua nini cha kufanya.

Aidha walisema ukosefu wa elimu ndio chanzo cha kuathiriwa na kemikali hizo huku wakiomba Serikali kuwasaidia kupata matibabu ya haraka kunusuru afya zao.



Jamal Baruti
Kaimu Mkurugenzi
- NEMC

ADA NA TOZO ZA MAZINGIRA...

Hatua hii ni mahsusi kurahisisha utendaji kazi wa Baraza hususani masuala ya Tathimini za Athari za Mazingira, Ukaguzi pamoja na utoaji elimu. Aidha, Ofisi za Kanda zimekuwa na mchango mkubwa katika jitihada zinazofanywa na Baraza

za ukusanyaji Ada na Tozo za mazingira. Hadi sasa Baraza lina jumla ya Ofisi za Kanda tisa (9) ambazo zinatoa huduma za mazingira kwa jamii.

Hitimisho

Kulipia tozo ni takwa mojawapo la Kisheria katika uzingatiji na utekelezaji wa Sheria. Hivyo, Baraza limeendelea kutoa elimu kwa njia ya radio, televisheni, magazeti na kwenye tovuti yake kuwakumbusha wawekezaji kukamilisha michakato ya EIA na EA na kuwakumbusha wawekezaji kuhakikisha wanakidhi matakwa ya Kisheria ikiwa ni pamoja na kusajili miradi mipya kwa ajili ya TAM na miradi iliyokuwepo kwa ajili ya Tathimini ya Ukaguzi wa Mazingira. Hii pia ikiambatana na ulipaji wa Tozo husika. Aidha, Baraza limeboresha Kanzidata ya wadaiwa na wadau wanaopaswa gharama za mapitio ya TAM na Tayari NEMC imejiunga na Mfumo wa malipo. Serikalini GEPG na hii inasadia katika kutambua wenye miradi ambao wanakuwa hawajalipia Tozo husika.

Baraza linasisitiza kuwa lengo kuu la Tozo za mazingira ni kusaidia watumiaji wa mazingira kuona thamani halisi ya mazingira anayoyatumia na faida anayoipata kutoka kwenye mazingira. Ada na Tozo za mazingira ni dhamana ambayo mchafuzi au mharibifu wa mazingira anatakiwa alipie gharama za uchafuzi katika mazingira (Polluter Pay Principle) inayomtaka kulipia anayechafua mazingira ili pesa inayopatikana iweze kusaidia wengine ambao hawachafui mazingira. Vilevile fedha inayopatikana kwenye Tozo inasaidia Baraza kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja kusimamia mazingira vizuri ili yaweze kudumu na kuwa salama kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Ofisi hizo za kanda ni kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali hapa chini:

Na.	MAKAO MAKUU	ANUANI
1	Ofisi Kuu ya Baraza, Dar es Salaam	Kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent S.L.P 63154, Dar es Salaam, Tanzania Simu: +255 22 2774852/4889, Nukushi +255 22 2774901 Barua pepe: dg.nemc.or.tz, Tovuti: www.nemc.or.tz
Na.	OFISI YA KANDA	ANUANI
1	Ofisi ya Kanda ya Ziwa ipo Mkoa wa Mwanza, Kanda hii hushughulikia mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Shinyanga na Geita,	PSSSF Front Wing, Ghorofa ya Sita, Kitalu Na. 17/1, 17/2 & 18, Barabara ya Kenyatta, S.L.P 11045. Mwanza
2	Ofisi ya Kanda ya Kaskazini ipo katika Mkoa wa Arusha. Kanda hii inajumuisha mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro,	Makongoro - Goliondoi Njiapanda, Ngorongoro Round About, Kitalu Na. 055019/1 & 055019/6, Jengo la Kituo cha Utalii Ngorongoro, Ghorofa ya Sita, S.L.P. 1041, Arusha Simu: +255738064966, Barua pepe: nemcarusha@nemc.or.tz
3	Ofisi ya Kanda za Juu Kusini ipo katika mkoa wa Mbeya. Kanda hii hushughulikia mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe.	Karume Avenue, S.L.P. Box 6215 Mbeya, Simu: +2552502469 Simu ya Mkononi : 0752215635 Barua pepe: nemcmbeya@nemc.or.tz
4	Ofisi ya Kanda ya Kati ipo katika mkoa wa Dodoma na hushughulikia mikoa ya Dodoma, Tabora na Singida,	Ghorofa ya Sita, Kambarage Tower, S.L.P 2724, Dodoma Simu: +255262963859/860 Barua pepe: nemcdodoma@nemc.or.tz
5	Ofisi ya Kanda ya Kusini ipo mkoani Mtwara na hushughulikia mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Lindi,	Eneo la Ligula, Barabara ya TANU, Ghorofa ya Kwanza, S.L.P 1259, Mtwara Simu: +255232334683. Barua pepe: nemcmtwara@nemc.or.tz
6	Ofisi ya Kanda ya Magharibi ipo Mkoani Kigoma na inafanya kazi katika mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa na Kagera.	Jengo la NSSF Mafao, Ghrofa ya Kwanza, Kitalu Na. 100 Block I, Mtaa wa Mnarani. S.L.P 974 Kigoma Ujiji, Barua pepe: nemckigoma@nemc.or.tz
7	Ofisi ya Kanda ya Mashariki (Kusini) ipo Mkoani Dar es Salaam na inasimamia maeneo ya Temeke, Ilala, Mkuranga, Kigamboni, Mafia, Kisarawe and Kibiti	Kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent S.L.P 63154, Dar es Salaam, Tanzania Simu: +255 22 2774852/4889 Nukushi +255 22 2774901 Barua pepe: dg.nemc.or.tz, Tovuti: www.nemc.or.tz
8	Ofisi ya Kanda ya Mashariki (Kaskazini) ipo mkoani Dar es Salaam na inasimamia maeneo ya Kinondoni, Ubungo, Bagamoyo, Chalinze,, Kibaha and Tanga	Kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent S.L.P 63154, Dar es Salaam, Tanzania Simu: +255 22 2774852/4889 Nukushi +255 22 2774901 Barua pepe: dg.nemc.or.tz Tovuti: www.nemc.or.tz
9	Ofisi ya Kanda ya Morogoro Rufiji	Jengo la NHC - 2D Complex, Orofa ya Pili Barabara ya Old DSM, P.O. Box 67106 Morogoro Simu: +255 22 2774852/4889, Nukushi +255 22 2774901 Barua pepe: dg.nemc.or.tz, Tovuti: www.nemc.or.tz



UMUHIMU WA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA (TAM) NA UANDAAJI WA MPANGO WA USIMAMIZI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA PALE MGODI UNAPOANZISHWA NA UNAPOFUNGWA . - DKT. GWAMAKA

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka aliyasema hayo alipofanya ziara kwenye mradi wa mgodi tarajiwa wa Nyanzaga uliopo Kata ya Igalula Wilaya ya Sengerema Mkoa wa Mwanza unaomilikiwa na Kampuni ya SOTTA MINING CORPORATION.

"Mgodi unapoanzishwa ni lazima ufanyiwe Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM) na mpango wa usimamizi na utunzaji wa mazingira kabla kuanzishwa na mpango wa ufungaji pale unapofungwa ili kulinda mazingira yetu." alisema Dkt. Gwamaka.

Dkt. Gwamaka alisema kuwa migodi iliyoanzishwa kabla ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inachangamoto nyingi ikiwa ni pamoja na migogoro ya kimazingira kati yake na jamii, pamoja na Serikali kuingia gharama kubwa ya kurekebisha mazingira yaliyoharibika na kuchafuliwa.

"Hasara nyingine ya kutokuweka mpango mkakati wa namna ya ufungaji wa migodi pindi unapofungwa ni pamoja na kuacha mazingira katika hatari kwa afya ya jamii na viumbe wengine hai." alisema Dkt. Gwamaka.

Ni mkakati wa Baraza kuhakikisha historia mbaya ya utunzaji wa mazingira kwa migodi iliyoanzishwa kabla ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 hayatajitokeza tena kwenye migodi itakayoanzishwa kwenye awamu hii ya Sita ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan.

Naye Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria kutoka NEMC, Mhandisi Redempta Samwel amepongeza hatua zinazochukuliwa na mradi wa



Watumishi kutoka NEMC wakiwa kwenye picha ya pamoja na wafanyakazi wa mgodi tarajiwa wa Nyanzaga uliopo Wilayani Sengerema Mkoa wa Mwanza unaomilikiwa na Kampuni ya Sotta Mining Corporation walipofanya ziara katika mgodi huo kukagua utekelezaji wa Sheria ya mazingira.

uchimbaji wa madini ya dhahabu wa Nyanzaga katika kuhakikisha mazingira yanatunzwa kuanzia hatua ya awali kabla ya shughuli za uchimbaji kuanza.

Pia, Mhandisi Redempta aliongeza kwa kusema kuwa Baraza lina wajibu na mamlaka ya Kisheria ya kufuatilia utekelezaji wa mpango mkakati ili kuepusha athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza.

"Ni muhimu kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kuandaa mpango wa usimamizi na utunzaji wa mazingira pale mgodi unapoanzishwa na unapofungwa." - Dkt. Gwamaka.

Wakati huo huo Meneja wa Kanda ya Ziwa Viktoria NEMC Ndg. Jerome Kayombo amesema mgodi tarajiwa wa Nyanzaga utakuwa ni wa mfano

kwa migodi mingine kwasababu umeanza ushirikiano mapema na wataalamu wa mazingira kuanzia hatua za mwanzo kabisa, hii itasaidia kuweka mipango mikakati ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka aliyasema hayo alipofanya ziara kwenye mradi wa mgodi tarajiwa wa Nyanzaga uliopo Kata ya Igalula Wilaya ya Sengerema, Mkoa wa Mwanza unaomilikiwa na Kampuni ya SOTTA MINING CORPORATION.

Wakati huo huo Meneja wa Kanda ya Ziwa Viktoria NEMC Jerome Kayombo amesema mgodi tarajiwa wa Nyanzaga utakuwa ni wa mfano kwa migodi mingine kwasababu umeanza ushirikiano na sisi wataalamu wa mazingira kuanzia hatua za mwanzo kabisa, hii itasaidia kuweka mipango mikakati ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

UHARIBIFU VYANZO VYA MAJI NA ATHARI ZAKE

UTANGULIZI

Nchi yetu imejaliwa kuwa na vyanzo vya maji vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na mito, maziwa, ardhi oevu na maji ya chini ya ardhi. Vyanzo vya maji ni rasilimali muhimu inayochangia maendeleo ya nchi, kwani tunapata maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzalisha nishati ya umeme, maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na shughuli mbalimbali za maendeleo nchini. Kutunza vyanzo vya maji ni kujiwekea mazingira mazuri ya kulinda afya ya jamii, kujenga uchumi endelevu wa nchi kwa ujumla.

UHARIBIFU WA VYANZO VYA MAJI NA ATHARI ZAKE

Licha ya kuwepo kwa Sheria za Usimamizi wa vyanzo vya maji (bahari, maziwa, mito, mabwawa, na chemchemi) kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji kutokana na kuwepo kwa shughuli za binadamu zinazofanyika pasipo kuzingatia Sheria zinazosimamia mazingira na rasilimali maji. Shughuli hizo ni pamoja na ukataji wa miti kwa ajili ya kujipatia kuni, mkaa au mahitaji ya ujenzi, mifugo, uchimbaji mchanga na madini, na ujenzi usiozingatia taratibu taratibu za mipango miji, kilimo kisicho endelevu. Pia shughuli za uchimbaji mchanga kwenye maeneo ya mito na uchimbaji madini kwenye vyanzo vya maji, kilimo na maogesho ya mifugo katika vyanzo hivyo vimekuwa vikichangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa vyanzo vya maji hususani kuongeza matope kwenye vyanzo vya maji. Vilevile uchepushaji wa maji kutoka katika vyanzo vya maji pasipo kuzingatia Sheria na taratibu zilizowekwa na Serikali za uchukuaji maji kwenye vyanzo vya maji (wenye vibali vya kuchota maji kuchukua maji zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa).

Vilevile, shughuli za binadamu zinachangia mabadiliko ya tabianchi (ongezeko la muda mrefu la joto la wastani la dunia) ambalo hupelekea kubadilika kwa mfumo mzima wa hali ya hewa. Mabadiliko ya Tabianchi ni tatizo linalokabili dunia katika karne ya ishiringi na moja na kutokana na athari zake katika nyanja mbalimbali. Aidha, mabadiliko ya tabia nchi yameathiri kwa kiasi kikubwa vyanzo vya maji na

kusababisha vyanzo hivyo kukauka na kupunguza uwezo wake wa kuzalisha maji na kupungua kwa ubora wa maji. Hali hizo zimeathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa maji kwenye maeneo mbalimbali nchini. Mfano mwaka 2021 mwishoni tumeshuhudia upungufu mkubwa wa maji katika bonde la Mto Wami/Ruvu ambalo ni tegemeo kubwa la maji yanayohudumia mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Changamoto hii inatokana na uharibifu uliokithiri wa mazingira katika bonde la Mto Ruvu. Uendelevu wa shughuli hizi pasipo kuzingatia Sheria kutaendelea kuathiri vyanzo cha maji hali ambayo itapelekea ukosekanaji wa ubora na wingi wa maji.

Athari nyingine zinazojitokeza kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji ni pamoja na ukosekanaji wa ubora na wingi wa maji ambayo ni tegemeo kwa wananchi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo na shughuli nyingine za maendeleo, mlipuko wa magonjwa kutokana na kutokuwa na majisafi na salama, kwani yatakokana au kuwa machache. Vilevile vyanzo vya maji vinaweza kuchafuliwa na viuatilifu vinavyotumika katika kilimo kwaajili ya kuu wadudu. Viuatilifu hivyo huingia kwenye maji na kusababisha ongezeko la magonjwa mengi yasiyotibika, kupungua kwa kina cha maji kwenye mito, kupotea kwa bioanuwai na uchafuzi wa maji. Hali hii husababisha kuongezeka kwa gharama ya kuchakata mali ghafi. Aidha maji yaliyochafuliwa huhitaji kiwango kikubwa cha madawa ya kutibu na kusafisha maji kutokana na uchafuzi wa mazingira katika vyanzo vya maji.

JITHADA ZINAZOTAKIWA KUKABILIANA NA ATHARI KWENYE VYANZO VYA MAJI

Suala la utunzaji wa vyanzo vya maji ni la kila mwanajamii, hii ni kuhakikisha kila mmoja anakuwa balozi mzuri wa kuona namna ya kuvilinda na kuvitunza vyanzo vya maji. Hivyo ni muhimu kila mmoja wetu kushirikiana kikamilifu katika kuhakikisha maeneo ya vyanzo vya maji hayachafuliwa na hayaharibiwi. Katika kutekeleza adhama hiyo, ni muhimu kwa kila taasisi na kila mmoja kuzingatia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake hasa zinazoelekeza kuhusu

uhifadhi wa vyanzo vya maji. Lengo ni kuhakikisha vyanzo vya maji vinakuwa endelevu.

Aidha taasisi husika zinatakiwa kuendelea kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Kuepuka kufanya shughuli mbalimbali za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji. Vilevile kutumia mbinu mbadala na endelevu za kilimo. Serikali za mitaa na vijiji kuwa na mipango madhubuti ya kutunza vyanzo vya maji kwenye maeneo yao kama kushirikiana na Wizara ya Mifugo kuhakikisha wafugaji wanajengewa mabirika na mabwawa ya kunyweshea mifugo kwani maji katika kipindi cha kiangazi yanakuwa machache ili wasiingie katika mito kunywesha mifugo yao. Pia kuanzisha Sheria ndogondogo za vijiji zitakazosaidia kusimamia rasilimalia maji katika vijiji husika.

Ili kuhakikisha ulinzi madhubuti wa vyanzo vya maji, kamati za ulinzi na usalama katika mikoa na wilaya zishiriki kikamilifu kwa kushirikiana na ofisi za mabonde ya maji katika kulinda vyanzo vya maji. Hii itahusisha vyombo vya dola kufanya operesheni za kushtukiza mara kwa mara kwani hii itasaidia kupunguza ama kuondokana na uchafuzi wa mazingira unaofanywa na watu kwenye vyanzo vya maji.

Baraza kama chombo cha kusimamia uhifadhi wa mazingira, limeshuhudia na kuona uharibifu na uchafuzi wa mazingira ukiendelea sehemu mbalimbali nchini na kusababisha athari mbalimbali kutokea. Vilevile Baraza limeendelea kujionea mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali yakifanyika, ukuaji wa miji na uanzishwaji wa miradi ukifanyika pasipo kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (Environmental Impact Assessment). Vilevile, mipango mingi inanzishwa pasipo kupitia mchakato muhimu wa Tathmini za Kimkakati ya Mazingira (Strategic Environmental Assessment) kwenye mipango hiyo kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu Na. 104 cha Sheria ya Mazingira.

Kwa kuzingatia umuhimu wa vyanzo vya maji na faida zake, Baraza linaisitiza kuhakikisha shughuli zote zinazoanzishwa kwenye maeneo hayo ziwe zimezingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira ikiwa ni pamoja na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa miradi inayoanzishwa, na vilevile kuhakikisha kuwa mipango ya maendeleo katika halmashauri iwe imefanyiwa Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na pia kuona jinsi gani Sheria ya Mita 60 inazingatiwa kwenye vyanzo vya maji kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu Na. 57 cha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC
Mhandisi Dkt. Samuel
Gwamaka akielezea namna ya
uhifadhi na utunzaji wa vyanzo
vya maji.



TUSHIRIKIANE KWA KARIBU KATIKA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZA KIMAZINGIRA- MHE. KHAMIS

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis alitembelea ofisi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kuahidi kuendelea kushirikiana kwa karibu na Baraza ili kuweza kutatua changamoto za kimazingira zinazowakabili wananchi.

Akizungumza mara baada ya kutembelea Ofisi za Makao Makuu ya NEMC Jijini Dar es Salaam, Mhe. Khamis amesema ameweza kufika NEMC kuona ni namna gani wanaweza kushirikiana katika jambo la usimamizi na ufanyaji wa tathmini ya kuona athari zinazoweza kusababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye mazingira.

"Kikubwa tumekuja kujifunza na kuona changamoto na kuzichukua na kuweza kuzisemea na kuzitafutia suluhisho na kuhakikisha wananchi wanaishi bila kuathirika na athari za mazingira. Kuna kazi kubwa ya kufanya ya kuhakikisha elimu inafika kwa wananchi ili kudhibiti uharibifu"-Mhe. Khamis.

Aidha Naibu Waziri alisema katika utoaji wa elimu ya mazingira kuna maeneo muhimu kama kwenye uchimbaji wa madini, elimu inatakiwa kuelekezwa zaidi ili kudhibiti uharibifu wa mazingira.

"Taaluma inahitajika kwa wananchi zikiwemo shughuli za uchimbaji wa



Mtumishi wa NEMC Bi. Florida Kavuli akimpa ua la ukaribisho Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Khamis Hamza Khamis baada ya kuwasili ofisi za NEMC zilizopo Mikocheni Jijini Dar es Salaam.

madini, shughuli za kwenye masoko na hata katika shughuli za kwenye misitu kwa sababu huko kinachofanyika watu bado hawana taaluma hii ya utunzaji wa mazingira. Aidha bado kuna harakati za uharibifu wa mazingira zinaendelea". Alisema Mhe. Khamis.

Naye Naibu Katibu Mkuu Bw. Edward Nyamanga amelipongeza Baraza kwa namna linavyoweza kukabiliana na changamoto nyingi zilizopo na

zinazoibuka kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Nashukuru tumekutana na Baraza, nimeweza kuzifahamu changamoto zinazowakabili na kuona kwa kiasi kikubwa linavyoweza kukabiliana na changamoto hizo, changamoto huwa zipo lakini kuna changamoto zinazoibuka nyingine kutokana na mabadiliko ya tabianchi."-Alisema Bw. Nyamanga.



Meneja Mawasiliano na Mahusiano kwa Umma – NEMC Bi. Irene John akielezea jambo kwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Khamis Hamza Khamis (Hayupo Pichani) alipowasili Ofisi za NEMC Mikocheni Jijini Dar es Salaam.



Watumishi wa NEMC wakisalimiana na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Khamis Hamza Khamis baada ya kuwasili katika ofisi za NEMC Mikocheni Jijini Dar es Salaam.

MRADI WA UHIMILI WA MABADILIKO YA TABIANCHI - PWANI ZA ZANZIBAR WAZINDULIWA



Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar Dkt. Omar D. Shajak na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka wakiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Warsha ya uzinduzi wa Mradi wa Kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii ya Pwani za Zanzibar.

Warsha ya mafunzo ya Mradi wa Kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii ya Pwani za Zanzibar ilifanyika wakati wa uzinduzi wa mradi. Warsha hiyo imefanyika katika ukumbi wa ASSP Maruhubi Mjini Zanzibar.

Warsha hiyo ilifunguliwa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar Dkt. Omar D. Shajak na kuhudhuliwa na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Gwamaka. Wengine walioshiriki katika warsha hiyo ni watumishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Watumishi wa NEMC na Viongozi kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali.

Dkt. Omar Shajak alisema kuwa mabadiliko ya Tabianchi ni janga la Kidunia hivyo, hatuna budi kukabiliana nayo. Alisema juhudi mbalimbali zimechukuliwa ili kupambana na mabadiliko hayo ikiwemo kuwepo kwa Sera, Sheria na mifumo ya Kitaasisi ya usimamizi wa mabadiliko ya Tabianchi.

Katika uzinduzi huo Dkt. Shajak aliishukuru na kuipongeza NEMC kwa juhudi kubwa inazozichukua katika kupatikana kwa fedha za mradi kupitia Mfuko wa Uhimili wa mabadiliko ya Tabianchi

(Adaptation Fund) ambao ulizinduliwa rasmi kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake, pia alilishukuru Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa UNDP kwani wao ndio chimbuko la kupatikana kwa andiko la mradi huu.

Kwa Upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka aliipongeza Zanzibar kupata fedha kwa ajili ya mradi wa kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii ya Pwani za Zanzibar kupitia Mfuko wa Adaptation Fund.

"Kuwa wa kwanza ni jambo linaloleta wajibu wa kuonesha mfano katika utekelezaji ili wanufaika watakaofuata waweze kujifunza. Siyo hivyo tu bali utekelezaji wenye ufanisi utavutia hata wafadhili wengine kuweka fedha zaidi kwenye mfuko kwa ajili ya kuendeleza kazi zilizoanzishwa na mradi huu sambamba na kulipatia Taifa letu sifa nzuri katika Jumuiya ya Kimataifa" alisisitiza Dkt. Gwamaka"

Dkt. Gwamaka alimaliza kwa kusema kuwa NEMC wataendelea kutoa ushirikiano na msaada wowote utakaohitajika kusudi mradi huu uweze kutekelezeka na kukamilika kwa wakati na mafanikio.

WAZIRI JAFU AAGIZA KILA MWANAFUNZI KUPANDA MTI NA KUUTUNZA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dkt. Selemani Jafo ameelekeza kila mwanafunzi apande mti, kuusimamia na kuutunza hatua itakayosaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Dkt. Jafo alitoa maelekezo hayo mnamo Januari 17, 2022 jijini Tanga wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua na kuhamasisha shughuli mbalimbali za hifadhi na utunzaji wa mazingira.

Alisema kuwa upungufu wa miti umekuwa chanzo cha kiwango cha mvua kupungua na joto kuongezeka kwa kasi hali inayosababisha ukame kupelekea kufa na kupotea kwa baadhi ya viumbe.

Kwa mantiki hiyo alisema kuwa kuna umuhimu wa kuwajengea utamaduni wa kupanda miti watoto wa shule ili kuwa na kizazi chenye kujali na kupenda mazingira.

"Pamoja na maelekezo ya Serikali ya kupanda miti milioni moja na nusu kwa kila halmashauri ambayo lengo ni miti milioni 276 kwa halmashauri zote 139 lakini kila mwanafunzi kuanzia chekecheke, msingi, sekondari akipanda mti mmoja na kuusimamia kwa mwaka mzima ndio utakuwa mkombozi wetu kukabiliana na changamoto hizi za kimazingira," alisema Mhe. Jafo.

Aidha, Waziri Jafo aliwaelekeza viongozi wa mikoa na wilaya kusimamia kikamilifu zoezi la usafi wa mazingira na kusema kuwa ni aibu kwa majiji makubwa kuwa machafu.

Alisisitiza kuwa maelekezo yaliyotolewa na viongozi wa kitaifa kuhusu usafi wa mazingira yatekelezwe na usafi katika siku za Jumamosi uwe ni utamaduni na uendelee kushika kasi.

Alitembelea pia dambo la kisasa la Jiji la Tanga ambapo alionesha kuridhishwa na namna wanavyoshughulikia taka ngumu na kuwapongeza viongozi wanaosimamia dambo hilo.

Hivyo, Waziri Jafo aliwataka viongozi wa Halmashauri nyingine ambazo zimenufaika na miradi ya ujenzi wa madambo ya kisasa kuhakikisha wanayasimamia ipasavyo.

Katika hatua nyingine Waziri Jafo alifanya ziara katika eneo la Chongoleani ambako kunakotarajiwa kujengwa bandari ya kupokelea mafuta ili kujiridhisha uzingatiaji wa maelekezo ya Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM).

Aliwataka wataalamu kutoka Wizara ya Nishati na wataalamu kutoka Mamlaka ya Bandari kuhakikisha masharti ya cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) yanazingatiwa ili mradi huo uwe endelevu na rafiki kwa mazingira.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiipanda mti akihamasisha jamii juu ya utunzaji na uhifahi wa Mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

ATHARI ZA UCHAFUZI WA MAZINGIRA ZITOKANAZO NA KELELE

Kelele ni sauti zilozidi kiwango kilichoruhusiwa na chenye kusababisha madhara kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira. Uchafuzi wa mazingira unatokana na kelele zisizozuilika au kudhibitiwa pale zinapozalishwa na kusababisha athari za kiafya kwa jamii. Kelele zinasababishwa na shughuli mbalimbali za viwanda, mipango isiyo endelevu ya miji kama kumbi za starehe na burudani, nyumba za ibada kuwa karibu na makazi ya watu, shughuli za kijamii kama harusi, sherehe, matamasha yakiwa yameambatana na matumizi ya vipaza sauti vyenye sauti za juu.

Athari za uchafuzi wa mazingira zitokanazo na kelele zimezidi kukua kwa kasi zaidi na kusababisha madhara kadha wa kadha hususan katika siku za hivi karibuni. Kuna athari mbalimbali za kelele ikiwa ni pamoja na kuathiri uwezo wa kawaida wa kuzungumza. kupunguza uwezo wa usikivu, kusababisha ulemavu kama uziwi, mabadiliko ya tabia na upungufu wa uwezo wa kuzaa unaosababishwa na msongo wa mawazo. Vilevile, kelele huathiri uwezo wa kujifunza na kutunza kumbukumbu, husababisha utoro, na hupelekea ongezeko katika matumizi ya madawa ya kujitibu

Aidha kelele kwa namna nyingine husababisha udhia, hofu, kichefuchefu, uchovu, huzuni, kutokuwa na uhakika, kutokujiamini, kutokuelewana, uwezo mdogo wa kufanya kazi, usumbufu wa usingizi ambapo hali hii husababisha kuwa na shinikizo la damu, mapigo ya moyo yasiyo ya kawaida hutokea (haraka au polepole), na kupunguza uwezo wa kufanya kazi. Vilevile kelele za papo hapo au muda mrefu na kwa kiwango cha juu hushtua neva na homoni hivyo kupelekea shinikizo la damu shubiri. Athari nyingine ni pamoja na maumivu ya kichwa, ubishi, mabadiliko ya hisia kwenye tendo la ndoa, kuongezeka kwa migogoro ya kijamii, ugonjwa wa "hysteria", na ugonjwa wa "psychosis", Kupungua ufanisi katika utendaji wa kazi kwa kuongezeka makosa, kupungua kwa motisha, kushindwa kukabiliana na kutatua matatizo.

Kelele huathiri viumbe wa nchi kavu na majini. Athari za kelele kwa mazingira na viumbe vyake ni pamoja na:- kuvunja mfumo wa kuzaa kwa viumbe (interference of reproduction); ndege kuhamisha makazi yao au wanyama kutoka kwenye maeneo yao waliyozoea kuishi na kuzuia kuzaliana kwao; Aidha Wanyama na ndege hupata wasiwasi na hofu na hivyo kuathiri tabia zao za upataji chakula, ukuaji na kuzaliana na wengine kufa; kusababisha kutoweka kwa viumbe (can be a path to extinction on the endangered species); uvuvi haramu na kutumia vifaa vya milipuko huzalisha mitetemo ambayo pia inaweza kuuwa samaki kwa wingi na kuharibu mazalia ya samaki. Pia kelele zinaweza kuathiri na kuvuruga usafiri wa majini (navigation);



Sehemu ya vyombo vya kupigia mziki vinavyochangia kelele katika mazingira.

Kutokana na athari nyingi zitokanazo na Kelele, Baraza la Taifa na Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limefanya kaguzi za mazingira katika maeneo mbalimbali na kuainisha changamoto zinazopelekea kuwepo kwa uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na kelele. Aidha, malalamiko mengi yamekuwepo kutoka sehemu za mijini ambako kuna ongezeko la watu likiambatana na uhaba wa makazi na ujenzi holela. Malalamiko ya kelele kutoka mijini ni kutokana na shughuli za binadamu za: - nyumba za starehe; biashara kama maduka, migahawa, wachoma nyama na chips, warekodi miziki; nyumba za ibada; viwanda; mikutano; maonyesho; matamasha; promosheni na burudani; matumizi ya vyombo vingine vinavyosababisha kelele kama pikipiki na magari.

Aidha, tatizo la kelele limeendelea kukua kutokana na Sheria za mipango miji na matumizi bora ya ardhi kutokuzingatia. Chanzo kikuu cha tatizo la kelele ni ukiukwaji wa Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka, 2007 na kusababisha malalamiko mengi.

Hali hii hupelekea kuwepo kwa shughuli zenye kelele karibu au ndani ya makazi ya watu. Aidha kwenye maeneo mengine mabadiliko ya matumizi ya ardhi yamefanyika pasipo kuzingatia utaratibu wa kushirikisha jamii husika, kuruhusu mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwa kipande cha ardhi kilichopo katikati ya makazi. Vilevile, miradi mingine yenye viashiria vya kelele imekuwa ikianzishwa pasipo kuzingatia matakwa ya Sheria za mazingira kama vile kufanya tathimini ya athari za mazingira. Hali hizi zimesababisha shughuli zenye kelele kuwa kwenye makazi ya watu, shule, na hospitali na hivyo kuleta malalamiko mengi.

Vilevile katika ufuatiliaji wa malalamiko ya wananchi kuhusu kelele, Baraza limebaini changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na 1) Kuwepo kwa vibali vya shughuli za kumbi za starehe vinavyotolewa

pasipo kuzingatia masharti ya eneo husika; 2) takwa la fomu kupitia kata husika kutokuzingatia na fomu kupitishwa kwenye kata tofauti na kumbi hizo zilipo; 3) kiwango kidogo cha uelewa wa masuala ya mazingira kwa jamii; 4) kukosekana kwa mipango ya usimamizi wa mazingira katika halmashauri na sekta; na 5) ushirikiano mdogo wa wadau katika shughuli za hifadhi ya mazingira.

Kwa kutambua adha na madhara ya kelele, Serikali imeandaa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali. Kelele na Mitetemo nchini ina dhibitiwa na Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za Mwaka, 2015 na kutangazwa kwenye Tangazo la Serikali (GN) Namba 32 la tarehe 30 Januari, 2015. Kanuni hizi zilitanguliwa na Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za Mwaka, 2013 na zilitangazwa kwenye Tangazo la Serikali (GN) Namba 204 la tarehe 28 Juni, 2013. Kanuni zote mbili zilitungwa kwa mujibu wa kifungu namba 230 (2) (s) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka, 2004.

Katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele na mitetemo Kanuni ya 11 ya Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za Mwaka, 2015 imeweka wazi kuhusu wajibu wa mtu yeyote anayezalisha kelele na mitetemo kwa kutumia njia yoyote iwezekanayo kudhibiti kelele anayozalisha na kuhakikisha hazididi kiwango kilichoainishwa katika jedwali la kwanza la Kanuni hizi.

Pamoja na makatazo hayo lakini pia Kanuni imeruhusu kiwango cha kelele na mitetemo kwenye mazingira kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na

Inaendelea Uk. 14 >>>

Mitetemo) za Mwaka, 2015 kwa kuzingatia Muda katika shughuli za kibinadamu kwenye Makazi ya watu,viwanda au karakana, shule/vyuo, maeneo ya kuabudia,maeneo ya ujenzi,mazingira ya kawaida, matangazo kwa kutumia vipaza sauti, sehemu za kumbi za starehe, kelele za vyombo vya usafiri pamoja na Migodi na Machimbo.

Vilevile suala la udhibiti wa kelele limepewa umuhimu wake na limewekwa na kuelekezwa kwenye Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 kifungu cha 53 (W) ambacho kinataja "Udhibiti wa Kelele" kama kero (nuisance) kadhalika sambamba na kifungu 53 vifungu 54 - 60 vinatoa nguvu kwa mamlaka (LGA), Mganga Mkuu Mkoa, Mganga Mkuu wa Wilaya na Afya ya Mazingira ambao ni maafisa walioidhinishwa (Authorized officers) kuingia na kukagua jengo lolote, kuondosha chukizo/kero, au hatari, kutoa ilani au maelekezo, kufunga biashara au huduma iliyo kero kwa jamii. Kinyume cha kutotekeleza vifungu vilivyotajwa wahusika hushitakiwa Mahakamani.

Baraza limendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji elimu kwa wadau kuhusu 1) Athari zitokanazo na uchafuzi wa kelele, 2) Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za Mwaka, 2015, na 3) Adhabu zilizoainishwa katika Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za Mwaka, 2015.

Jitihada nyingine zinazofanywa na Baraza ni pamoja na kufanya kaguzi katika maeneo kadhaa ikijumuisha baa na kumbi za starehe; nyumba za ibada; viwanda; saluni; warekodi miziki; matamasha; promosheni na burudani mbalimbali. Kaguzi hizo huambatana na upimaji wa viwango vya kelele ambapo vililinganishwa na viwango vinavyoruhusiwa ambavyo vimebainishwa kwenye Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za mwaka, 2015.

Aidha, kaguzi hizo zilibainisha kuwa wadau wengi uelewa wao ni mdogo na hivyo kuwaelimisha, kuwapa maonyo na kuwaelekeza hatua za kuchukua ikiwa ni pamoja na kupunguza kelele. Hatua zinazochukuliwa kwa wale wasiozingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni za Usimamizi wa Viwango vya Ubora vya Mazingira (Udhibiti wa Kelele na Mitetemo) za mwaka, 2015 ni pamoja na:- maonyo; Amri ya kizuizi kwenye shughuli zenye madhara makubwa kwa mazingira; na Amri ya kutimiza masharti ya mazingira.

Hivyo basi kila mtu au Taasisi zinaaswa kufanya shughuli zake kwa kuzingatia Sheria na Miongozo ya nchi, pia mawasiliano baina ya taasisi ni muhimu sana ikiwa ni pamoja na kushirikiana kwa pamoja kuhifadhi na kulinda mazingira kwa ustawi wa maisha ya jamii, kukuza uelewa kwa jamii kwenye masuala ya mazingira na mwisho kuna umuhimu wa kujijengea uwezo taasisi au watu binafsi ili kuhakikisha usimamizi madhubuti wa masuala ya mazingira unafanyika.

WAZIRI JAFU AZINDUA BODI YA NEMC JIJINI DODOMA, ATOA MAAGIZO



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo akimkabidhi kitendea kazi Mwenyekiti wa Bodi ya Nane ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Prof. Esnati Chaggu mara baada ya kuizindua bodi hiyo leo Februari 4, 2022 jijini Dodoma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dkt. Selemani Jafo ameiagiza Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kupitia muundo na majukumu ya Baraza hilo ili kuangalia utekelezaji wake.

Aidha aliagiza kuhakikisha mfumo wa vibali vya taka hatarishi unatengenezwa ndani ya siku 45.

Maagizo hayo aliyatoa Februari 4, 2022 jijini Dodoma wakati akizindua Bodi ya Nane ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na kuikabidhi vitendea kazi ili kutekeleza majukumu yake ya kiutendaji.

Dkt. Jafo alisema kuwa bodi ya NEMC ni chombo muhimu kinachoishauri Serikali katika masuala muhimu ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

"Namtaka Mwenyekiti wa Bodi hii kuhakikisha anasimamia suala la mfumo na ndani ya siku 45 mchakato wa mfumo huo uwe umekamilika," alisema Dk. Jafo

Waziri Jafo alitaka Bodi hiyo, kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mazingira ya Mwaka 2021, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Serikali.

Aliaagiza kuupitia upya muundo na majukumu ya Baraza ili kuimarisha utendaji wake na kutatua changamoto zilizopo katika suala zima la uhifadhi na usimamizi wa mazingira na kutoa ushauri ipasavyo.

"Kama mnavyofahamu Sera Mpya ya Mazingira ya mwaka 2021 inategemea kuzinduliwa Februari 12, mwaka 2022 na sera hii inatoa miongozo ya kiseru katika kutatua changamoto mpya za mazingira zinazoikabili nchi yetu," alisema

Aidha aliwataka kusimamia mapato na matumizi ya fedha na kulisimamia vema Baraza kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais ili miongozo inayotolewa na Ofisi itekelezwe kwa weledi.

Kwa upande wake Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Mary Maganga amempongeza Mwenyekiti Prof. Esnati Chaggu na wajumbe wa Bodi hiyo kwa kuchaguliwa kuongoza Taasisi hiyo yenye jukumu kubwa la kusimamia masuala ya mazingira Nchini.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Mhandisi Esnati Chaggu, aliahidi kufanyia kazi maelekezo ya Waziri na kuishauri Serikali katika masuala muhimu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

FAHAMU FURSA NA CHANGAMOTO ZA TAKA NGUMU MKOA WA DAR ES SALAAM

Takataka ni uchafu ambao unatokana na mabaki ya vitu baada ya kuzalishwa au kutumika ambao hauwezi kutumika tena bila ya kurejelezwa kwa matumizi mengine. Taka hizo huzalishwa majumbani, viwandani na maeneo ya biashara. Watu wengi huamini na kujenga dhana kuwa takataka ni uchafu ambao hauwezi kutumika tena kwa matumizi mengine hali iliyopelekea kuwa na taka nyingi kushinda uwezo wa miundo mbinu iliyopo. Aidha, jamii inakumbushwa kuwa kuna fursa nyingi zitokanazo na taka hizo.

Ili kuweza kutambua fursa zitokanazo na takataka tunatakiwa kutambua aina za takataka ambazo zinazalishwa katika jamii yetu. Tutambue kuwa kuna aina tatu za takataka ikiwemo taka ngumu, taka maji na taka gesi.

Katika kudhibiti taka ngumu Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake imetoa mamlaka katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nchini kusimamia Sheria hiyo. Pamoja na Sheria hiyo kuwa wazi na kutoa mamlaka katika Halmashauri na Serikali za Mitaa kuhusu udhibiti wa taka ngumu, lakini bado kuna changamoto nyingi katika usimamizi.

Mkoa wa Dar es Salaam kwa mfano, ni Mkoa wa kibiashara na ni Mkoa wenye watu wengi kuliko mikoa mingine yote nchini. Hali ya usafi wa jiji la Dar es Salaam hususani udhibiti wa taka ngumu ni tatizo la muda mrefu ambalo lina changamoto nyingi.

Jamii ya wakazi wa Dar es Salaam miongoni mwao wamekuwa na tabia ya utupaji wa taka katika maeneo yasiyo rasmi, tabia hii imechangia kwa kiasi kikubwa jiji kuwa chafu na kusababisha madhara mbalimbali kwa afya ya binadamu na mazingira katika jamii ikiwemo magonjwa kama vile kipindupindu, kuhara, kutapika, kansa, pamoja na uharibifu wa vyanzo vya maji na mafuriko.

FURSA ZINAZOTOKANA NA TAKA NGUMU

Kama tunavyojua kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ni Mkoa wa kibiashara ambao una fursa nyingi ya upatikanaji wa viwanda ndani yake, ni Mkoa wenye watu wengi kutokana na hili taka nyingi kutoka majumbani na katika shughuli za kijamii ikiwemo kilimo, ofisini, viwandani, masoko, madukani, taasisi za kiserikali huzalishwa. Taka hizo nyingi hutupwa kwenye madampo na nyingine huchomwa kwenye maeneo ya makazi. Wananchi wanatakiwa watambue kuwa sio kila kitu kinachotambulika kama takataka kinatakiwa kiishie kutupwa kwenye madampo, bali taka hizo zinaweza kutumika na kuwa fursa kubwa ya kujipatia kipato na kuweza kuendesha maisha yao.

Taka ngumu huweza kuwa fursa endapo

zitachambuliwa kuanzia sehemu ya uzalishaji mpaka mtu wa mwisho anayetumia bidhaa mfano mabaki ya chakula huweza kutumika kulishia mifugo kama paka, mbwa na nguruwe. Aidha, mabaki hayo yanaweza kutumika kuzalisha gesi na mbolea. Kwa upande mwingine taka za plastiki kama chupa na ndoo vinaweza kutumika kwa ajili ya kuwekea maua au kuuza katika viwanda vinavyoweza kurejeleza. Taka za chuma chakavu au nyaya za umeme zilizochakaa zinaweza kukusanywa pamoja na kuuzwa katika viwanda husika.

Umuhimu wa kutumia takataka zinazozalishwa kwa matumizi mengine umezingatiwa kwa kiasi kikubwa na Baraza la Taifa ka Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Hivi karibuni kwa mfano, Mkuruzi Mkuu NEMC, Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka alisema kuwa takataka isiwe kero bali iwe ni mojawapo ya chanzo cha kujipatia kipato na kuweza kupunguza mzigo katika madampo yetu. Ameeleza kuwa ili kuweza kuchangamkia fursa hiyo tunatakiwa kujua taka ambazo tunazalisha majumbani zinatakiwa kutenganishwa na sio kuchanganywa. Endapo zitachanganywa zitasababisha kushindwa kuchambuliwa na kuweka ugumu wa uteketezaji katika madampo yetu.

Dkt. Gwamaka alieleza kuwa Sheria ya Mazingira imewapa mamlaka Halmashauri, Wilaya na Serikali za Mitaa kusimamia zoezi la ukusanyaji, uhifadhi na usafirishaji wa taka hizo. Ingawa NEMC imetajwa kwenye Kanuni lakini wasimamizi wakuu ni Halmashauri, Manispaa na Serikali za Mitaa.

Aliendelea kusema kuwa pia Sheria ya Mazingira imemtambua na kumpa nguvu mkaguzi wa mazingira ambaye anateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya mazingira. Wakaguzi hao wapo

wilaya na mikoa yote kwa ajili ya kusimamia shughuli za utunzaji wa mazingira.

Dkt. Gwamaka alisema kuwa utupaji wa taka hovyo katika maeneo mbalimbali mkoani wa Dar es Salaam umekithiri hivyo kunafanyika jitihada mbalimbali ya kuhakikisha Maafisa Mazingira wa Halmashauri na watendaji wa Serikali ya Mitaa wanapewa elimu ya mazingira ili kupanua uelewa, kwani kero kubwa zinazotoka kwa jamii yetu ni kutokana na kutoelewa Sheria ya Mazingira na Kanuni mbalimbali zinazo ratibu utendaji.

Katika kutafuta msingi wa kuweza kutatua changamoto na malalamiko yanayoletwa na wananchi, NEMC iliandaa warsha ya kutoa elimu kwa viongozi na watendaji wa Kata na Mtaa katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa lengo la kupata suluhisho ili kuweka ustawi wa mazingira katika maeneo husika. Pia lengo la warsha hiyo ni kuwaelekeza majukumu ya kisheria na kiutendaji pamoja na kuweka mahusiano ya karibu na Baraza katika kutatua changamoto za kimazingira katika jamii.

Umuhimu wa elimu kwa jamii ni kutokana na NEMC kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu wa changamoto wanazopata katika ukusanyaji wa taka kuna baadhi ya maeneo wanakaa na taka kwa muda mrefu bila ya kukusanywa na jamii ikifahamu kuwa suala la ukusanyaji wa taka za majumbani ni la NEMC. Sheria imetaja NEMC kuwa msimamizi lakini msimamizi mkuu wa taka hizo ni Halmashauri, Manispaa na Serikali za Mitaa katika mikoa. Hivyo kuweza kupunguza changamoto katika ukusanyaji Mwananchi unatakiwa kuzitenganisha taka hizo kabla ya kwenda kutupwa kwenye madampo kwa ajili ya uteketezaji. Tumia fursa za taka kujiongeza kipato.



Sehemu ya Taka ngumu zilizochambuliwa na kuwa fursa ya kipato

ATHARI ZA MAZINGIRA KATIKA MAENEO YA MIGODI



Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka (wa pili kulia), akiwa katika ziara ya kukagua mazingira katika mgodi wa madini ya dhahabu wa Bulyanhulu Mkoani Geita, akiwa ameambatana na Afisa wa NEMC kanda ya Ziwa Tanganyika Dkt. Befrina Igulu (wa pili kushoto) na Kaimu Meneja Kanda ya Ziwa Victoria Bwa. Jerome Kayombo (kulia).

Utangulizi

Binadamu wanapofanya vitendo kadhaa kwenye mazingira athari za aina mbalimbali huweza kutokea. Athari hizi zinaweza kuwa mbaya au nzuri ingawa neno "athari" hufanya iweze kuonekana kuwa ni kitu hasi. Ikiwa hatua tunayochukua kwenye mazingira ni kitu kinacho toa faida itakuwa chanya. Lakini ikiwa kinachafua au kuharibu tutasema kuwa athari hiyo ni hasi.

Sekta ya Madini ni moja kati ya sekta muhimu katika ukaji wa uchumi wa nchi na inapewa kipaumbele katika mpango wa Taifa wa kukuza uchumi wa viwanda. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017, uchimbaji madini nchini umegawanyika katika makundi matatu ambayo ni Uchimbaji Mkubwa, Uchimbaji wa Kati na Uchimbaji Mdogo. Makundi haya yamegawanywa kwa kuzingatia leseni ya uchimbaji.

Athari zitokanazo na Uchimbaji na Uchenjuaji wa Madini

Uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za uchimbaji wa madini umegawanyika katika makundi kadhaa. Uharibifu wa mazingira unaweza kuelezewa kwa kuzingatia aina ya madini yanayochimbwa, eneo ambapo uchimbaji unafanyika au mifumo ya uchenjuaji inayotumika.

Shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu huzalisha taka sumu ambazo ni chanzo kikubwa cha uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Tatizo la uchafuzi wa mazingira hususani kwa wachimbaji wadogo husababishwa matumizi ya teknolojia duni na zisizo salama kwa mazingira, uelewa mdogo wa sheria na wachimbaji hawa kutokuona umuhimu wa hifadhi ya

mazingira.

Wachimbaji wadogo pamoja na wakubwa wa madini wana athari zinazofanana kwenye mazingira. Kutokana na kaguzi mbalimbali zilizofanywa na Baraza athari za kimazingira kwenye maeneo ya uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu zinachangiwa na mambo yafuatayo:

- Kuondoa uoto wa asili kutokana ukataji miti ovyo kwa ajili ya kupata maeneo ya kufungua migodi na kuimarisha mashimo ya uchimbaji;
- Kuacha mashimo bila kuyarekebisha au kuyafukia mara upatikanaji wa madini unapopungua;
- Kuzalisha kelele na vumbi kwa wingi kwenye maeneo ya kusagia mawe ya madini ("locally made crushers" and "ball mills");
- Matumizi kemikali za kuchenjua dhahabu yasiyozingatia hifadhi ya mazingira
- Uwezo duni wa kudhibiti maji yamvua yaliyopitia katika vifusi vilivyo na kemikali ("washouts from tailings with remnant processing chemicals");
- Kushindwa kudhibiti taka ngumu na majitaka yatokanayo na shughuli za uchimbaji kwenye maeneo ya Mdogo;
- Uelewa mdogo kwa wachimbaji wa madini kuhusu uhifadhi wa mazingira;
- Kukosekana kwa mifumo madhubuti ya ufungaji migodi inayomilikiwa na wachimbaji wadogo,
- uchafuzi wa mazingira na vyanzo vya maji;
- Asidi kutoka kwenye miamba kutiririka kwenye maji yaliyo ardhini;

- Upotezaji wa bioanuwai;
- matumizi makubwa ya maji; na
- Shughuli za uchimbaji pia zinaweza kuchochea migogoro na kutishia haki za binadamu ikiwa ulinzi hautafikiwa au kama hautasimamiwa vyema.

Aidha, athari nyingi za kimazingira katika migodi hutokana na shughuli zenyewe za uchimbaji wa madini hasa usiozingatia mpango wa uthibiti wa mazingira wakati wa uendeshaji migodi na pia kutokuwepo kwa mpango wa uendeshaji mgodi (Mine Plan). Ifahamike kuwa mpango wa usimamizi na ufutilaji wa mazingira (Environmental Management and Monitoring Plan) huandaliwa mapema wakati wa andiko la TAM (Tathmini ya Athari kwa Mazingira). Athari zingine zinazoendana na mazingira ni athari za kijamii. Baadhi ya migodi midogo imebainika kutumikisha watoto walio umri wa chini ya miaka kumi na nane (18) katika shughuli za uchimbaji, hivyo kupelekea muitikio mdogo wa kielimu katika maeneo yenye migodi mingi midogo.

Sheria zinazosimamia masuala ya mazingira kwenye Shughuli za Madini

Uchimbaji madini Tanzania unaongozwa na Sheria ya madini ya Mwaka 2010 ikisomwa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017. Aidha, Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inahusika kwa kuwa shughuli za uchimbaji madini zinaathiri mazingira, hasa katika miradi mikubwa ya uchimbaji inayohitaji kufanyika kwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira TAM kabla ya uchimbaji kuanza.

Ili kuweza kuondokana na athari za mazingira katika migodi, ni lazima sheria husika zizingatiwe na pia kuhakikisha kuwa kuna mipango madhubuti itakayowapa wachimbaji wadogo riziki mbadala au hisa za kiuchumi ili waweze kufanya uchimbaji wa madini kwa kuzingatia Sheria za uhifadhi wa mazingira. Katika maeneo ambayo uchimbaji wa madini ni halali, mbinu halali ni pamoja na kujadiliana kuhusu kusimamia na kutekeleza mpango usimamizi na ufutilaji wa mazingira (Environmental Management and Monitoring Plan) kama ulivyoainishwa kwenye andiko la Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

Vilevile Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linasimamia utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika menea ya migodi kwa kuhakikisha ahadi ya kukuza na kupitisha utendaji bora wa Kanuni za maadili juu ya usimamizi wa topesumu (tailings) na mpango endelevu wa jinsi ya kufunga mgodi (mining closure plans), kuhakikisha migodi inajitolea katika kuimarishwa kwa uwazi na kushiriki habari na hasa kushiriki taarifa kuhusu utendaji wao wa mazingira na mifumo na jamii zilizoathirika, kuhakikisha kuwa matumizi bora ya mifumo ya malalamiko ya jamii (Grievance Redress mechanisms) ipo na inafanya kazi,

Kuhakikisha ahadi ya kutii Kanuni ya mchafuzi

Inaendelea Uk. 17 >>>

ATHARI ZA MAZINGIRA KATIKA ...



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka, akikagua mitambo ya utafiti chini ya mgodi wa takribani kilomita 1.5 kutoka usawa wa ardhi katika mgodi wa Bulyanhulu Mkoani Geita.

hulipa (Polluters Pay Principle), inayofungamana na kurekebisha uharibifu wa mazingira unaotokana na hitilafu kwa kulipia gharama zinazohusiana na shughuli, Kuhakikisha kuwa ahadi kutoka kwa waendeshaji wa sekta ya uchimbaji madini wa kiwango cha kati na kikubwa kupitisha programu za ufanisi wa nishati (kama vile vitengo vya kurejesha joto taka, mafunzo ya wafanyakazi, ukaguzi wa mara kwa mara wa matengenezo, vifaa vya ufanisi wa nishati nk.) pamoja na kuhakikisha usimamizi salama wa kemikali (hasa sayanaidi) ambazo hutumika kurejesha na kuchakata miamba yenye madini (ores).

Katika suala hilo kwa ujumla Baraza limekuwa likikutana na changamoto kubwa hasa kwa wachimbaji wadogo wanaomiliki leseni ndogo za uchimbaji (PML) kutofanya zoezi la Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na hata wanaofanya TAM hawafuati utaratibu wa kitaalam wa usimamizi wa mazingira wakati wa uchimbaji wa madini ulioelekezwa katika andiko hilo la TAM ya mgodi husika. Migodi Mingi midogo haijaajiri wataalam wa mazingira ambao wanawajibwa wakusimamia utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira katika kipindi chote cha maisha ya mgodi (Life of Mine-LoM).

Kwa upande wa migodi ya kati na ile mikubwa changamoto nyingi za kimazingira zinatokana na kutokuzingatia usanifu mzuri wa mgodi hasa katika miondombinu ya kuhifadhi taka hatarishi zitokanazo na uchenjuaji wa madini na shughuli nzima za kiuchimbaji mfano ni usanifu mbovu wa mabwawa ya kuhifadhi tope (Tailings Storage Facility) yanayotoka katika mitambo ya uchenjuaji wa madini (Processing Plant) hivyo kupelekea uchafuzi wa udongo na vyanzo ya maji.

Changamoto nyingine ni utelekezaji wa migodi midogo pasi na kufanyiwa Environmental Restoration/ rehabilitation. Wachimbaji wengi wasio rasmi (Artisanal Miners) pamoja na wachimbaji wadogo pindi migodi yao inapofikia ukomo wa uzalishaji ikiwa ina maana madini yaliyokuwa yamekusudiwa yamekwisha, huitetekeza migodi ikiwa na uharibifu mkubwa wa kimazingira. Yote haya hutokea sababu hawakuwa na mpango madhubuti wa kusimamia mazingira wakati wa uchimbaji wa madini.

Jithada zinazofanywa na Baraza

Kaguzi mbalimbali kuangalia kiwango uzingatiaji

Sheria na pia uchafuzi na uharibifu wa mazingira zimefanywa kwenye migodi n.k. Kaguzi hizi zimefanyika kujua ni kwa kiasi gani miradi hiyo inavyozingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya mazingira. Taasisi zilizokaguliwa zimepewa maelekezo ili kuzingatia Sheria na kuboresha hali za kimazingira.

Baraza pia linapokea malalamiko kuhusu uchafuzi wa mazingira katika shughuli za uchimbaji madini na kuyashughulikia kwa kutumia njia mbalimbali. Baraza linapokea malalamiko linatuma maofisa kwenda eneo husika kutathmini kiwango cha uharibifu kilichofanyika ili kuweza kuchukua hatua stahiki kutatua tatizo hilo.

Baraza limefanya jitihada za kuelimisha wananchi kuhusu usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Wananchi wanaovunja Sheria za Mazingira huelimishwa kwanza na pale inapotokea hali hiyo kujirudia tena, Baraza linachukua hatua za Kisheria ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini mbalimbali. Mtuhamiwa kashindwa kulipa faini, hatua zaidi za Kisheria zinachukuliwa dhidi yake.

Kuhimiza shughuli zinazoanzishwa kwa sasa zizingatie tathmini ya athari za kimazingira *Environmental Impact Assessment (EIA)*, na wale ambao shughuli zao zilianza kabla Sheria ya

mazingira haijaundwa wafanye tathmini ya uhakiki wa athari ya mazingira *Environmental Audit (EA)*. Utoaji elimu na mafunzo kwa ajili ya maofisa kutoka idara mbali mbali za Serikali katika suala zima la ukaguzi wa mazingira na uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya mazingira.

Kuhamasisha viongozi, wafanyakazi, wafanyabiashara na wananchi kuisoma na kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA 2004), Miongozo na Kanuni za Mazingira. Pia Baraza limesisitiza kwa Halmashauri kuunda Sheria ndogondogo za mazingira "Bylaws" za Halmashauri ambazo zinakidhi masuala yaliyopo katika maeneo husika.

Kusisitiza wenye migodi kuwa na mifumo madhubuti ya kushughulikia taka ngumu na kusafisha majitaka kabla hayajaruhusiwa kurudi kwenye mazingira.

Kuandaa mikutano ya mara kwa mara kuwashirikisha wadau katika shughuli mbalimbali ili kuelimishana kuhusu masuala ya kimazingira na Sheria ya mazingira.

Baraza kwa kushirikiana na taasisi husika liliandaa andiko la mradi ("Project Proposal) wenye lengo la kupunguza Athari za Kimazingira na Kiafya kwa Wachimbaji Wadogo wa dhahabu. Andiko, hilo la mradi wenye thamani ya US\$ 7.33 Mil. liliidhinishwa na kupatiwa fedha. Tayari mradi huo umeanza kutekelezwa

Baraza limetoa mafunzo kwa Wakaguzi wa Mazingira (Environmental Inspectors) kutokea katika taasisi mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na Halmashauri za miji na Wilaya, Wizara ya Maji, Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Hifadhi ya Ngorongoro, Wizara ya Afya, na Maafisa kutoka Baraza. Wakaguzi hawa wana jukumu la kusimamia uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ikiwa ni pamoja na shughuli za uchimbaji mdogo wa madini.

Baraza limeendelea kutoa mafunzo na kufuatilia utendaji wa washauri elekezi (EIA/EA Experts) pamoja na Kampuni za ushauri (EIA/EA Consultancy Firms), ambao wana jukumu la kutoa elimu na miongozo ya kitaalamu kwa wawekezaji kwenye shughuli mbalimbali zikiwemo na madini.



Mkurugenzi Mkuu wa NEMC akizungumza na wafanyakazi wa mgodi wa dhahabu wa Buzwagi uliopo Wilaya ya Kahama Mkoa wa Shinyanga baada ya kuwasili katika mgodi huo.

CHANGAMOTO YA MAGUGU MAJI ZIWA BABATI KUTATULIWA

Ziwa Babati lipo katika mji wa Babati Mkoa wa Manyara, ni miongoni mwa bonde la ufa la Afrika Mashariki. Ziwa lina ukubwa wa kilomita za mraba 18, maji yake ni baridi na yanakusanywa kutoka kwenye chemchem za chini ya ardhi na vilima vilivyolizunguka ziwa hilo. Katika upande wa Kaskazini Mashariki mwa ziwa Babati kuna mlima Kwaraa na msitu wa Ufyomi.

Hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya magugu maji yaliyoota kwa wingi kwenye maeneo ya ziwa yenye kina kifupi cha maji na kusambaa kwa haraka sana mpaka kwenye kina kirefu. Hali hii ilisadikiwa kuathiri kiwango na ubora wa maji na kuathiri mazingira na maisha ya viumbe waishio majini. Pia shughuli za kiuchumi na kijamii zinazofanywa kupitia ziwa hilo kama vile uvuvi na usafirishaji wa majini. Sambamba na hilo ziwa Babati linakabiliwa na changamoto ya uharibifu wa mifumo ya kiikolojia kutokana na matumizi yasiyokua endelevu ya rasilimali zinazopatikana katika ziwa hilo.

Kutokana na changamoto hizo, Halmashauri ilitoa taarifa katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ili waweze kuwasaidia kuondoa magugu hayo na kuwapa ushauri wa kitaalamu wa namna wanavyoweza kupunguza au kuyaondoa kabisa magugu maji hayo pamoja na kudhibiti uharibifu wa ikolojia ya ziwa hilo.

NEMC iliandaa timu ya wataalamu kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Sekretarieti ya mkoa na Halmashauri ya Mji wa Babati kwa ajili ya

kufanya utafiti katika ziwa Babati ili kubaini chanzo cha magugu maji kuota na kusambaa kwa kasi, athari ya magugu katika ikolojia ya ziwa na jamii inayozunguka. Katika hili wataalamu walijikita kuainisha na kutathmini athari hasi zinazosababishwa na shughuli za binadamu.

Katika kufanya tafiti, wataalamu hao walijikita kuangalia shughuli mbalimbali zinazofanywa na binadamu zinazochangia kuongezeka kwa magugu maji, waliangalia jinsi magugu maji yaliyoota kuzunguka ziwa na ndani ya ziwa na walifanya majadiliano na jamii inayozunguka ziwa ili kuona shughuli zinazoendelea na kuathiri ustawi wa ziwa pamoja na kubuni mbinu za kitaalamu zinazoweza kuzingatiwa ili kudhibiti uharibifu wa ziwa.

Kupitia utafiti huo waliweza kubaini mambo yafuatayo:

Shughuli za kibinadamu kama kilimo zinachangia kuharibu ustawi wa ziwa kutokana na kutokufuata Sheria ya mita sitini (60) kutoka chanzo cha maji, shughuli za ufugaji zinachangia uchafuzi wa maji kutokana na unyweshaji wa mifugo moja kwa moja na kulisha mifugo kwenye ziwa na kusababisha tope na mazingira rafiki kwa magugu maji kustawi, uvuvi haramu unachangia kuchafua maji, kuathiri viumbe wa majini na uchumi. lakini pia kuongezeka kwa magugu maji, kukata miti kwenye hifadhi iliyokaribu na ziwa kwa ajili ya kuchomea tofali, shughuli za kutengeneza tofali na ufugaji nyuki, kuoga, kufua na kuosha vyombo ndani ya ziwa.

Eneo kubwa la ziwa limetawaliwa na magugu maji, kuanzia kwenye fukwe na kusambaa

mpaka kina cha mita 3. Ingawa kuna magugu yanaonekana kuendelea kusambaa mpaka kina cha ziwa cha chini zaidi.

Mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutokana na ongezeko la watu na mifugo ambapo watu wanalazimika kutafuta maeneo kwa ajili ya kilimo na machungio. Kwa wastani maeneo ya kilimo na makazi yameongezeka kwa asilimia 3.1%, na makazi 4.9% kati ya mwaka 2000 na 2001. Na maeneo ya machungio yamepungua kwa asilimia 5.3%. Shughuli zote hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la tope na mazingira rafiki kwa magugu maji kukua na kusambaa kwa kasi.

Aidha katika utafiti huo wataalamu waliweza kutambua athari zinazosababishwa na magugu maji katika ziwa Babati ambazo ni magugu maji kutanda na kufunika sehemu kubwa ya maji na kufanya ukubwa wa ziwa kupungua, shida ya upatikanaji wa samaki, kutoa mianya ya uvuvi haramu, yanapunguza ubora wa maji kwani yakioza yanachangia kutengeneza tope na kupunguza kina cha maji na shughuli za usafirishaji wa majini, na pia ni maficho ya watengenezaji wa pombe haramu.

Hata hivyo kuna jitihada mbalimbali za wazi zinazofanywa na Halmashauri ya Babati ili kuhakikisha ziwa linalindwa na kutunzwa Pamoja na rasilimali zake. Jitihada hizo ni kuhakikisha wavuvi wote wana vibali na leseni za uvuvi, kutoa elimu kwa jamii inayolizunguka ziwa kuhusu athari zinazoweza kusababishwa na shughuli za kibinadamu na kuwepo kwa hifadhi misitu na milima kuzunguka eneo hilo.

Pamoja na jitihada hizo, timu ya wataalamu



Picha ikionesha magugu maji (Maranda) katika ziwa Babati



walipendekeza hatua mbalimbali ambazo zinaweza kutumika ili kudhibiti magugu maji. Hatua hizo ni kama ifuatavyo; kudhibiti mmonyoko wa udongo kwa kupanda miti, kuweka mipaka, kulima kilimo cha matuta, kudhibiti virutubisho vinavyopelekea ustawi wa magugu maji, kutoa elimu na kuanzisha Sheria ndogondogo. Hatua hizi zitahusisha utoaji wa elimu ya mazingira, kupitia mara kwa mara mpango wa matumizi bora ya ardhi, kufunga ziwa kipindi cha mzaano na kutekeleza Sera ya mazingira na uvuvi.

Jitihada za Baraza za kuongoa Mfumo wa Ikolojia ya Ziwa Babati

Katika jitihada za kuboresha mazingira mifumo ya Ziwa Babati, Baraza lilishirikiana na wadau kuandika andiko na kuwasilisha kwa wadau wa maendeleo (Adaptation Fund) kwa ajili ya maombi ya fedha. Aidha, Baraza limeendelea

kusubiria maamuzi ya *Adaptation Fund* kuhusu uidhinishaji wa fedha. Mradi huo ni kuongoa ziwa Babati ili kuongeza uhimili wa mabadiliko ya tabianchi wilayani Babati (Restoration of Lake Babati for Enhanced Climate Change Adaptation in Babati District). Aidha, lengo kuu la mradi ni kuongoa mfumo ikolojia wa ziwa Babati ulioharibiwa na kujenga uwezo kwa jamii inayolizunguka ziwa kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Shughuli za mradi zitahusisha yafuatayo:

1. Kuhamasisha njia za kudhibiti mmonyoko wa udongo maeneo ya juu ya dakio la ziwa (upstream of the lake catchment);
2. Kuondoa magugu maji na tope ndani ya ziwa;
3. Kuweka mipaka ya ziwa na uzio ili

Picha ikionesha shughuli mbalimbali za kibinadamu zinazoathiri ikolojia ya ziwa Babati

kuongeza uhifadhi wa ziwa na kupunguza mwingiliano wa binadamu na viboko ;

4. Kuwezesha shughuli za kujipatia kipato kwa wananchi wanaozunguka ziwa, ambazo ni rafiki kwa mazingira na himilivu kwa athari za mabadiliko ya tabianchi; na
5. Kujenga uwezo wa kitaasisi kwa Halmashauri ya Wilaya Babati na jamii inayozunguka ziwa, katika kutekeleza mikakati ya kuongoa ziwa, kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kusambaza taarifa za matokeo ya mradi.

HABARI PICHA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Seleman Jafo akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali kutoka Ofisi ya Makamu Rais Pamoja na Wajumbe wa bodi mpya ya NEMC.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka alipotembelea mgodi wa Katavi Mining Co. Ltd uliopo Mkoa wa Katavi kukagua utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika mgodi huo.



Uhifadhi wa maeneo oevu katika hifadhi ya Taifa ya Katavi ni njia ya kuhakikishia viumbe hai kama viboko kuendelea



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka wa pili kutoka kulia akipokea maelezo kutoka kwa mmoja wa viongozi wa Mkoa wa Katavi alipotembelea Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi kupata taarifa kuhusu uhifadhi na utunzaji wa mazingira katika Mkoa huo.



kuishi katika mazingira salama.
TUTUNZE NA KUHIFADHI
MAENEO OEVU ILI KUTUNZA
IKOLOJIA.




Watumishi kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa mgodi wa Katavi Mining Co. Ltd mara baada ya kutembelea mgodi huo kukagua uhifadhi na utunzaji wa mazingira katika mgodi huo.

HABARI PICHA: MAONESHU YA KIMATAIFA



Banda la NEMC nchini Qatar lilitembelewa na Balozi wa Tanzania (katikati) Mh. Dkt. Mahadh Maalim pamoja na balozi wa Kenya (wa pili kulia) nchini Qatar Mh. Paddy Ahenda wamepongeza NEMC kwa kushiriki maonesho makubwa ya Kimataifa ya Kilimo na Mazingira na kuwashauri waendeleo kutumia fursa kama hizi ili kutoa elimu na kuitangaza nchi kupitia hifadhi na utunzaji wa Mazingira.



Baadhhi ya zawadi zilikuwa zinatolewa na NEMC



Meneja Kanda ya Ziwa Victoria Bw. Jarome Kayombo wakibadilishana ujuzi na Technolojia ya Uhifadhi wa taka zitokanazo na mabaki ya chakula (Food Waste) kwenda kutengeneza mbolea.



Elimu kwa Wateja inaendelea

YA MAZINGIRA - QATAR (10 - 14 Machi, 2022)



Picha ya pamoja Kati ya wawakilishi wa NEMC pamoja na wawakilishi wa Kampuni ya ORKA Trading inayopatikana nchini Qatar inayojishughulisha na utengenezaji na uuzaji wa sensors mbalimbali kwa ajili ya kutambua uchafu na ubora katika mazingira



NEMC imetembelea Kampuni ya **Elite Paper Recruiting** ya nchini Qatar inayojishughulisha na urejerezaji wa taka za karatasi. Kampuni hii inakusanya taka za karatasi toka maeneo mbalimbali nchini Qatar na kuzirejereza ili kupata bidhaa za karatasi hivyo kupunguza ukataji wa miti kiholela. Kwa kufanya hivyo inatunza Mazingira hususani kukabiliana na changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi. Kampuni hii inasambaza bidhaa zake katika mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania, hivyo ni fursa nzuri kwa Tanzania kupitia NEMC kushirikiana nao kuanzisha viwanda vya kurejereza taka za karatasi kwa kutunza Mazingira na kuongeza fursa za ajira nchini.



Baadhi ya washiriki wa Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo na Mazingira yaliyofanyika nchini Qatar wakiwa katika picha ya pamoja kwenye Banda la NEMC na mwekezaji wa Kampuni ya Amir Hamza ambayo pia amewekeza nchini Tanzania mara baada ya kupata Elimu ya Mazingira.



Wateja waliotembelea Banda la NEMC kwenye maonesho ya Kimataifa ya Kilimo na Mazingira jijini Doha nchini Qatar wakiendelea kupata elimu na kuscan namba maalum kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali kuhusu NEMC

KAULI YA MAZINGIRA YETU

Jumanne 23 JANUARI 2022



“Baadhi ya taka hatarishi hulipuka na kusababisha moto. Nyingine ni kemikali au sumu zinazoweza kujeruhi au kuaa. Utupaji hovy wa taka hizi husababisha madhara makubwa kwa afya na uhai wa binadamu na mazingira kwa ujumla. Chukua tahadhari kwa kutozishika au kukaa karibu nazo kuepuka madhara yake.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU

Jumanne 23 JANUARI 2022



“Taka hatarishi zina fursa ya kiblashara ndani na nje ya nchi kutokana na uwezo wake wa kurejereza. Pia husaidia kupunguza athari ya taka hizi katika mazingira, afya na maisha ya binadamu sambamba na kutunza mazingira. Hivyo tumia fursa hii kwa kuziua na kujiongeza kipato.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU


JUMANNE Tarehe 4 JANUARI 2022



“Mfumo wa ikolojia uliopo katika Hifadhi ya milima ya Livingstone una mchango mkubwa katika kupunguza hewa ukaa. Hivyo kuchoma moto na kukata miti ovyo katika milima hiyo ni sababu inayochangia uzalishaji wa hewa ukaa.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMANNE 11 JANUARI 2022



“Maeneo oevu ni lazima yatunzwe na kulindwa kwa ukaribu ili kuhakikisha yanakuwa endelevu. Katika kutekeleza azma hiyo Tanzania imeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha maeneo hayo yanatunzwa na kulindwa kikamilifu.”

TU琳DE NA KUITUNZA ARDHI OEVU

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMANNE 18 JANUARI 2022



“Uwepo wa hifadhi katika milima ya livingstone hupelekea kuwa na hali ya hewa safi katika wilaya ya Kyela na maeneo yanayozunguka, pia milima hiyo inachangia kuvuta mvua za kutosha ukilinganisha na maeneo mengine ambayo inaruhaba wa misitu, hivyo tunapoharibu hifadhi ya misitu katika milima ya Livingstone husababisha upotevu wa hewa nzuri na mvua kutonyesha.”

TUNZA MAZINGIRA NA YENYWE YAKUTUNZE

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMANNE 23 JANUARI 2022



“Utaditi umebaini kuwa mifuko ya asili ambayo siyo plastiki matumizi yake ni endelevu na inaweza kutumika mara nyingi na kufanyiwa urejereaji (recycling) jambo ambalo haliwezekani katika mifuko ya plastiki hivyo tumia mifuko mbadala ili uweze kutunza mazingira.”

CHUKUA MAZINGIRA KWA KUTUMIA MIFUKO MBADALA

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMANNE 18 JANUARI 2022



“Mifuko ya plastiki ni mifuko ambayo haozi na ni hatari kwa viumbe hai na mazingira kwa ujumla, hivyo tumia mifuko rafiki kwa mazingira kama vile mifuko ya karatasi, vikapu na mifuko ya vitamba.”

TUMIA MIFUKO MBADALA KUTUNZA MAZINGIRA

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMAA 21, JANUARI 2022



“ Kutokana na madhara makubwa ya mifuko ya plastiki ni vema wafanyabiashara kuacha kuzalisha, kusambaza, kuuza na kutumia mifuko ya plastiki badala yake waanze kuuza mifuko ya karatasi na vikapu vya asili kwa ajili ya kutunza mazingira.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU

Jumatatu 24 JANUARI 2022



“ Taka hatarishi ni taka zinazotakana na madawa ya kilimo, hospitali na mifugo yaliyoisha muda wake, taka za kemikali za majumbani na viwandani, vifaa chakavu, taka za migodini, betri chakavu, mafuta machafu, taka za kielekitroniki, taka za mionzi, yuma chakavu, matairi chakavu. Fuata taribu za Kisheria (omba vibali) katika kukusanya, kusafirisha, kuhifadhi na kuteketeza.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU


“ Miamba ya matumbawe ipo ndani ya maji ya bahari na inatengenezwa na viembe waitwomatumbawe "coral polyps". Viembe hawa wanaishi pamoja na mmea (algae) na hutengeneza chakula kwa kutumia mwanga yaani "photosynthesis". Miamba ya matumbawe inajengwa na madini ya kalsiamu kaboneti (CaCO₃) kama uchafu (end product) utokanao na viembe hawa ambapo miamba hili hulinda miji yao. Epuka uvuvi haramu kuhifadhi matumbawe.”



FAHAMU SABABU ZA UHARIBIFU WA MATUMBWE

KAULI YA MAZINGIRA YETU

“ Miamba ya matumbawe huathirika na shughuli za kibinadamu ikiwemo uvuvi haramu wa kutumia mabomu na nyenzo ambazo hazikubaliki, uchimbaji mafuta na gesi baharini, uchimbaji mchanga ambao husababisha kujaa kwa mchanga na udongo n.k. Hivyo tufanye shughuli zetu kwa kufuata Sheria ili kuzuia uharibifu wa miamba ya matumbawe.”



KAULI YA MAZINGIRA YETU

Jumatatu 24 JANUARI 2022



“ Milima ya Livingstone ni kichocheo cha upatikanaji wa maji katika vyanzo vya maji vilivyopo katika maeneo yanayozunguka milima hiyo ikiwemo mto Ruaha na Ziwa Nyasa.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMATANO, 13 JANUARI 2022



TAMBUA UMUHIMU WA MAENEO OEVU

UMUHIMU WA MAENEO OEVU

“ Maeneo oevu yana bioanuwai adimu sana hapa duniani ambazo aghalabu hupatikana maeneo hayo tu.
• Ni vyanzo vikuu vya maji katika maeneo mengi duniani yanayotumika kuzalisha umeme, kunywesha mifugo, kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya nyumbani.
• Maeneo oevu yanatumika kwa shughuli za kimila na kiatalii.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU

ALHAMISI 13 JANUARI 2022



YATUNZE MAENEO OEVU

“ Ardhi oevu husaidia kuchuja maji yanayokusanyika wakati wa mvua nyingi na kudhibiti mafuriko, lakini pia husaidia kuchuja uchafu na sumu kwenye maji. Epuka kufanya shughuli za kibinadamu katika maeneo oevu ili kuendelea kulinda ikolojia ya maeneo haya.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMAA 13 JANUARI 2022



“ Kwa mujibu wa katozo la mifuko na vifungashio vya plastiki, usajili wa leseni na vibali kwa ajili ya kulagiza ndani ya nchi, kusafirisha nje ya nchi, kuzalisha na kuuza mifuko ya plastiki lazima viwango vinavyokubalika Kisheria vizingatiwe.”

ZINGATIA VIWANGO VINAVYOKUBALIKA KISHERIA

KAULI YA MAZINGIRA YETU

JUMATATO 17 JANUARI 2022



TUMBA MIFUKO NA VIFUNGASHIO VINAVYOKUBALIKA KISHERIA.

“ Mifuko na vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango Kisheria vina athari kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira kwa ujumla. Ni marufuku kuingiza, kuzalisha, kusambaza, kuuza na kutumia mifuko na vifungashio visivyokidhi viwango vilivyowekwa Kisheria.”

KAULI YA MAZINGIRA YETU


JUMATANO 13 JANUARI 2022




TUATUNZE MAENEO OEVU KWA AJILI YA KUZALISA MIAMBO

“ Kwa kutambua umuhimu wa ardhi oevu, Tanzania ilisaini mkataba wa Kimataifa wa Ramsar (Ramsar Convention) msamo tarehe 02 Februari 1971 katika mji wa Ramsar nchini Iran. Lengo ni kuongeza umakini katika ulinzi wa maeneo haya na kuhakikisha yanakuwa endelevu. Hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kuangana na Serikali kuyalinda na kuyatunza maeneo oevu.”

KATUNI







Kwa mawasiliano zaidi;

Mkurugenzi Mkuu,

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),

35 Mtaa wa Regent/Migombani, Kitalu Na. 29/30, S.L.P 63154, Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 277 4852/4889, +255 713 608 930, Nukushi: +255 22 277 4901

Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www.nemc.or.tz

Namba ya Bure: 0800110116

   @nemctanzania

 NemcTVTanzania

 www.nemc.or.tz

#MazingiraYetuUhaiWetu